3000/=

# UCHANGANUZI SEMANTIKI WA MANENO MKOPO YA KIKAMBA KUTOKA KISWAHILI

**TASNIFU**

**YA**

**JANE MUMBUA DAVID**

**ILIYOTOLEWA KWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**2009**

David,Jane Mumbua
*Uchanganuzi semantiki wa maneno mkopo ya kikamba*
2009/333471

KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

## IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote

______________________________

**JANE MUMBUA DAVID**

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta, kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi

______________________________

**DAKTARI ALICE NYAMBURA MWIHAKI**

______________________________

**PROFESA IRERI MBAABU**

## TABARUKU

Tasnifu hii nawatabarukia wafuatao:

**Mume wangu**

'Davies' ulinifaa kwa hali na mali

Nilipochelea kuogelea, ulinihimiza

Tangulizi tulianza nawe, tamati tumetia kikomo. 'Nî mũvea'

**Wanangu**

Mwongela, Wangare na Nzoli

Kwa dhati mlinikumbusha na kunihimiza: "mum fanya homework yako teacher asikuchape". Asanteni kwa himizo lenu.

**Babangu Marehemu**

Nzoli Nthale uliotesha ndoto ya elimu nyoyoni zetu.

Kwa makini ukaikuza na kuipalilia.

Ndoto ilikua na kumea mabawa. Thax 2 God.

## SHUKRANI

Shukrani kwa Mola kwa kunijalia afya na uwezo wa kuikamilisha kazi hii.

Tajiriba na uzoevu wangu wa lugha wanikosesha maneno mwafaka ya kuwashukuru wote waliohusika kufanikisha kazi hii. Moyo hautatulia nisipowataja wachache, wengine nikiwashukuru kwa jumla.

Wasimamizi wangu Dkt Mwihaki na Prof Mbaabu hamkujipa pumziko hadi kazi ilipokamilika. Mlidhihirisha uwajibikaji wa hali ya juu kama wasimamizi wangu kwa kunihimiza, kunielekeza na kunikosoa. Mungu awazidishie wema na kupanua mipaka yenu ya utajiri wa lugha.

Namshukuru Bi Gatheji kwa mawaidha yake ambayo yalinifaa nilipokuwa naiteua mada yangu na kuitetea.

Shukrani zangu pia ziwaendee wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa kunipa motisha katika kazi hii hususan Dkt Mathooko, Dkt Richard Wafula, Dkt Masinde na Dkt Momanyi. Zaidi nawashukuru Bw. J. P. Mugambi na Dkt. Ndungo kwa kunichochea kufanya shahada ya pili.

Wanafunzi wenzangu hasa tulioshirikiana kukitegua kitendawili cha nadharia ya 'SAM' Saraha, Ngugi na Njurai. Asanteni kwa ushiriiano wenu.

Aidha ningependa kuishukuru jamii ya Mwongela kwa jumla. Kwa hali na mali mlinihimiza kuikamilisha kazi yangu. Nilipotatanika kufasili maana kamili za maneno ya Kikamba hamkusita kunielekeza. Asante 'ũkũlũ' (Baba Mkubwa).

Mamawangu Mpendwa Julia Wangare. Shukrani kwa kunifafanulia utamaduni wa Wakamba ambao ulinifaa kufasili baadhi ya maana ya maeno. Nĩ wega!

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

| | |
|---|---|
| Mchakato : | Namna ya kufanyika kwa jambo fulani |
| Sarufi Amilishi Mfumo: | Nadharia ya sarufi inayotazama lugha kama mfumo wa maana unaowakilishwa katika matini ya kisarufi |
| Tahakiki Usemi : | Nadharia ya isimujamii inayotazama lugha kama mfumo wa uzoevu wa kijamii katika muktadha wa utamaduni. |
| Utafsiri : | Mchakato ambao matini hufasiriwa na wanajamii. |
| Utohozi : | Utaratibu wa kuyabadili maumbo ya maneno. yaliyokopwa kutoka lugha changizi moja hadi nyingine ili yaafiki vikwazo vya mfumo wa lugha pokezi. |
| Ukopaji : | Mchakato wa lugha moja kuhamisha kipashio kutoka lugha nyingine. |
| Uzalishaji : | Mchakato ambao kupitia kwake, matini hutolewa na wanajamii. |
| Vikoa maana : | Nyanja za maana za kileksika kulingana na sifa za kisemantiki. |
| Viwakilishi dhana : | Hifadhi ya maana inayoshirikiwa na wanajamii lugha. |

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| T U | : | Tahakiki Usemi |
| SAM | : | Sarufi Amilishi Mfumo |
| Taz | : | Tazama |
| uk. | : | Ukurasa |

# IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kuchanganua mchakato wa kisemantiki kwa kuegemea maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Uchanganuzi huu hasa ulilenga kubainisha kanuni zinazotawala taratibu mbalimbali za utohozi maana. Tafiti awali zimeangazia zaidi utohozi fonolojia na utohozi mofolojia bila kuzingatia kanuni katika mchakato wa utohozi maana. Aidha kazi hii ilinuia kufidia upungufu wa tafiti awali kwa dhamira ya kupanua ufahamu zaidi katika mfumo wa maana, na semantiki ya Kikamba. Utafiti ulifuata nadharia msingi ya Tahakiki Usemi na kushirikisha Sarufi Amilishi Mfumo. Kwa jumla nadharia hizi hutazama lugha kama mfumo wenye maana na unaodhibitiwa na mfumo wa kijamii. Utafiti huu pia ulihusisha njia mbili kuu za utafiti: utafiti wa nyanjani na ule wa maktabani. Tasnifu ya utafiti imewasilishwa kwa njia ya maelezo, mifano na vielezo katika sura nne.

Sura ya kwanza maswala ya kimsingi yanajitokeza: usuli wa mada, swala la utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, tahakiki ya maandishi, misingi ya nadharia na uchanganuzi wa data. Sifa za kifonolojia, kimofolojia na kisemantiki zimeangaziwa katika sura ya pili yaani muundo wa maneno ya Kikamba. Matokeo kuhusu taratibu za utohozi semantiki na kanuni husika katika maneno mkopo yaliyochanganuliwa yamefafanuliwa katika sura ya tatu. Jumla ya mahitimisho, matokeo ya utafiti na mapendekezo ya utafiti yamejadiliwa katika sura ya nne. Imani na falsafa za kijamii ni miongoni mwa maswala yaliyodhihirika kuelekeza maana za maneno mkopo.

## YALIYOMO

**Vitangulizi** **Ukurasa**

Mada....................i

Ikirari....................ii

Tabaruku....................iii

Shukran....................iv

Dhana muhimu....................v

Vifupisho....................vi

Ikisiri....................vii

Yaliyomo....................viii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**....................1

1.0 Usuli wa Mada....................1

1.1 Swala la Utafiti....................4

1.2 Malengo ya Utafiti....................5

1.3 Maswali ya Utafiti....................6

1.4 Tahadhania za Utafiti....................6

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti....................6

1.6 Sababu za Kuchagua Mada....................8

1.7 Tahakiki ya Maandishi....................10

1.7.1 Maandishi kwa Jumla Kuhusu Ukopaji....................10

1.7.2 Maandishi ya Jumla Kuhusu Utohozi....................12

1.7.3 Maandishi ya Jumla Kuhusu Utohozi Katika Lugha za Kibantu....................14

1.7.4 Tafiti Bayana Kuhusu Utohozi Katika Lugha za Kibantu....................15

1.8.0 Misingi ya Kinadharia....................17

1.8.1 Tahakiki Usemi....................17

1.8.2 Sarufi Amilishi Mfumo....................22

1.9.0 Mbinu za Utafiti....................25

1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data....................26

1.9.2 Mbinu za Uchanganuzi wa Data.........................................28
1.9.3 Mbinu za Uwasilishaji wa Data.........................................29

**SURA YA PILI: MUUNDO WA MANENO YA KIKAMBA.................30**
2.1 Muundo wa Kifonolojia.........................................30
2.1.1 Fonimu za Kikamba.........................................31
2.1.2 Vokali za Kikamba.........................................32
2.1.3 Konsonanti za Kikamba.........................................36
2.1.4 Silabi za Kikamba.........................................40
2.1.5 Toni Katika Lugha ya Kikamba.........................................43
2.2 Muundo wa Kimofolojia.........................................45
2.2.1 Nomino za Kikamba.........................................45
2..2.2 Uundaji wa Nomino.........................................47
2.2.2.1 Nomino Kutokana na Vitenzi.........................................48
2.2.2.2 Nomino Kutokana na Vivumishi.........................................49
2.2.2.3 Nomino Kutokana na Majina Mengine.........................................49
2.3 Muundo wa Kisemantiki.........................................50
2.3.1 Muundo wa Leksimu.........................................51
2.3.2 Mahusiano ya Fahiwa.........................................53
2.3.3 Vikoa Maana.........................................56
2.3.5 Ualama.........................................58
2.3.6 Dhana ya Muktadha.........................................60

**SURA YA TATU: MISINGI YA UTOHOZI MAANA.........................63**
3.1 Kanuni Utohozi Maana .........................................63
3.1.1 Kanuni za Kiisimu .........................................64
3.1.2 Kanuni za Kijamii .........................................69
3.1.3 Kanuni za Kihistoria.. .........................................73
3.2.0 Taratibu za Utohozi Maana .........................................76

3.2.1 Ufinyizi Maana ........................................................................76
3.2.2 Usogezi Maana ........................................................................85
3.2.3 Upanukaji Maana ....................................................................95
3.2.4 Urari wa Umbo.......................................................................101

**SURA YA NNE: HITIMISHO**..........................................................105
4.1 Matokeo ya Utafiti.................................................................... 109
4.2 Mahitimisho ya Utafiti..............................................................116
4.3 Mapendekezo ya Tafiti Zaidi.....................................................117
**Marejeleo**...........................................................................................119

**Kiambatisho**.......................................................................................... 122

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli wa Mada

Utohozi maneno mkopo unashughulikiwa kuegemea taaluma ya isimu linganishi historia (Taz Anttila 1972, Bynon 1977 na Hock 1986). Isimu linganishi historia hutegemea hoja mbili za kimsingi: lugha hudhihirisha ulinganifu wa kimaumbo na kimaana, na lugha zote duniani huwa katika hali ya mabadiliko. Chanzo cha mabadiliko huwa mahitaj i ya ukuaji wa lugha kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine mtagusano wa lugha.

Mtagusano wa lugha husababishwa na mahusiano ya kijamii kama vile shughuli za kibiashara au maingiliano ya kitamaduni (Taz Lyons 1992, Bynon 1996 na Crowley 1997). Wataalamu wamebaini kuwa, mtagusano wa lugha hutokea sana katika shughuli za kibiashara, ambapo bidhaa husambaa na majina yake. Kwa jumla, lugha zinapotagusana tunapata matokeo mbalimbali. Baadhi ya matokeo haya ni pamoja na uwili lugha, ukopaji, kujinasibisha na kuhamisha lugha. Utafiti wetu ulilenga ukopaji wa leksia unaosababishwa na mtagusano wa lugha. Ni wazi, mtagusano wa lugha hudhihirisha pia mtagusano wa kitamaduni. Licha ya lugha kutumika kama chombo cha mawasiliano, wataalamu wengi huiona kama chombo cha kuendeleza utamaduni wa jamii yoyote ile.

Utamaduni wa jamii fulani, hufinyanga mazingira ambamo jamii hiyo inaishi kwa kutumia lugha. Utamaduni huo huelezwa na kusambazwa kwa kutumia lugha. Kwa vile

hakuna jamii mbili zilizolingana na kuwa sawa kitamaduni, katika hali ya mtagusano huwa vigumu lugha moja kueleza kikamilifu dhana iliyo katika lugha ya pili. Ni katika hali kama hizi ndipo lugha hulazimika kukopa maneno kutoka lugha nyingine kwa minajili ya kueleza mambo mapya yasiyopatikana katika lugha hizo. Kwa mfano, si rahisi kuzungumzia uvuvi bila kutafakari mazingira ya bahari, ziwa au mto. Kazi hii basi iliangazia maingiliano kati ya Kikamba na Kiswahili ambamo utamaduni ulichukuliwa kuwa kipengele muhimu katika mchakato wa ukopaji.

Tulivyotangulia kusema, ukopaji ni ule mchakato wa lugha moja (pokezi) kuhamisha kipashio kutoka lugha nyingine (changizi). Maneno yaliyohamishwa huitwa maneno mkopo. Kuna ukubalifu miongoni mwa wanaisimu kuwa, ukopaji si wa kileksika tu, bali pia fonimu, mofimu za kisarufi au ruwaza za kisintaksia (Taz Bynon 1977 na Campbell 1996). Hata hivyo, ni vyema tutaje kuwa ukopaji wa kileksia hutokea zaidi kwani mfumo wa leksia ni kiwakilishi cha utamaduni wa lugha husika. Maneno hayakopwi kiholela bali hufuata mbinu tofauti: kukopa kwa tafsiri, kukopa kwa sisisi na kutohoa. Utafiti huu ulitalii maneno mkopo ya kileksia kwa kuegemea utohozi semantiki.

Kwa kawaida, lugha haikopi kanuni ila maumbo au maana; ndio sababu utohozi hutokea. Utohozi ni utaratibu wa kuyabadili maumbo au maana za maneno yaliyokopwa kutoka lugha changizi ili yalingane na kuafiki mfumo wa lugha pokezi. Utohozi wa maneno mkopo hutokea ili kanuni za lugha zisibadilike kupitia ukopaji. Dhana ya utohozi hudhihirika katika mawanda maalumu ya lugha kama vile: fonolojia, mofolojia na

semantiki. Utohozi fonolojia hutokea ili neno litamkike kulingana na kanuni za lugha kopaji. Kwa upande wa mofolojia, maneno mkopo sharti yazingatie kanuni za kisintaktiki ili yakubalike katika lugha pokezi. Kimsingi, maneno mkopo hutoholewa kupitia taratibu za utohozi maana. Taratibu za utohozi maana nazo huelekezwa na kanuni za kiisimu, kijamii, kitamaduni na kisaikolojia.

Tunafahamu leksia hazijitokezi ubongoni mwa mzungumzaji kiholela ila hupangika katika ruwaza maalumu (Taz Anttila 1972 na Lyons 1977). Mpangilio huo umewabidi wanaisimu kuzungumzia muundo wa kisemantiki ambao hunguzia dhana ya vikoa maana na ualama. Neno mkopo basi katika mfumo wa lugha lazima liathiri mfumo awali wa kisemantiki. Kwa mfano, miongoni mwa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili ni *mama* "mzazi wa kike" ambalo ni kisawe cha *mwaitũ* Hapo awali neno *mwaitũ* lilirejelea mzazi wa kike. Baada ya neno "mama" kukopwa, neno *mwaitũ* limechukua nafasi ya ualama maana na pia ualama msambao. Utohozi semantiki kwa hivyo ni mchakato ambao uhusisha dhana ambazo huingiliana na kufungamana kwa karibu sana.

Tawi la semantiki kwa jumla halijakua kiasi cha matawi mengine ya kisarufi (Taz Anttila 1972, Bynon 1996, Mcmahon 1996, na Habwe na Karanja 2004). Baadhi ya wataalamu wametaja dhana hizi za utohozi semantiki pasipo kudhihirisha jinsi zinavyojitokeza katika maneno mkopo. Rai hii ilichochea lengo la kutalii utohozi semantiki, hasa kwa kuzingatia mtagusano wa kitamaduni kwa kipindi kirefu baina ya Kikamba na Kiswahili.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Mtagusano kati ya Kikamba na Kiswahili tangu enzi za biashara ya masafa marefu umedhihirisha ukopaji mwingi uliofuatwa na kaida za utohozi semantiki.

Lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili zimeingiliana kwa zaidi ya karne moja. Kuwepo kwa magofu ya nyumba, majengo ya kanisa, na makaburi sehemu za Ikutha Kitui Kusini kwadhihirisha kuwepo kwa wamishonari kutoka pwani miaka ya 1896 (Taz Hofmann 1931, Mbaabu 1996, na Ogot 1976). Wamishonari hao na wasafiri wengine wa kibiashara walitumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana na wenyeji. Ni wazi maeneo haya tangu zama zile hadi leo yamekopa zaidi na hasa utamaduni na dini. Aidha maeneo haya yamekopa majina ya mimea kutoka pwani (kwa mfano: 'mnazi' – *mũnathi*) pamoja na yale ya vifaa vingine vya kitamanduni.

Utafiti nyanjani ulidhihirisha lugha ya Kikamba imezidi kukopa kutoka lugha ya Kiswahili. Ukopaji huu umezingatia kanuni mbili za ukopaji wa leksia kuwa: ukopaji leksia husambaa kutoka lugha yenye hadhi ya juu hadi lugha ya hadhi ya chini, na lugha hukopa sana majina ya dhana zinazozuka katika msambao wa kitamaduni (Taz Hock 1986). Mtagusano huu wa Kikamba na Kiswahili umechanganuliwa katika misingi ya kisayansi kwa lengo la kufafanua utohozi maana kwa undani na michakato yake.

## 1.1 Swala la Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kuchanganua utohozi semantiki katika mfumo wa lugha ya Kikamba kwa lengo la kutathmini kanuni na taratibu za utohozi semantiki. Tafiti awali

zilishughulikia miundo na utohozi kiwango cha fonolojia na mofolojia katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Kazi hii basi, ilidhamiria kufidia tafiti awali kwa kufafanua semantiki ya Kikamba, kuchanganua taratibu za utohozi maana na kubainisha kanuni zilizoelekeza taratibu za utohozi maana katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili.

Athari za maneno mkopo katika muundo wa kisemantiki wa lugha ya Kikamba ni jambo ambalo halingeweza kuepukika katika uchanganuzi wetu. Kama tulivyodokeza, dhana katika mchakato wa utohozi semantiki huingiliana na kukamilishana. Dhana zilizochanganuliwa zilionekana kufungamana mno kiisimu kama tulivyodhihirisha katika kazi hii. Kanuni zilizobainishwa ziliangazia maswala ya kijamii kama vile miiko na imani na hivyo kufanya utifiti huu kuwa muhimu katika kumulika mahusiano ya kijamii miongoni mwa jamii ya Wakamba. Juhudi za kutalii swala la utafiti zilituelekeza kuwa na malengo yafuatayo ya utafiti.

### 1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo bayana manne:

1. Kuainisha maneno mkopo kulingana na vikoa maana.
2. Kutathmini kanuni za utohozi maana zinazoelekeza taratibu za utohozi maana wa maneno mkopo.
3. Kujadili athari za maneno mkopo katika mfumo leksia.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Malengo bayana yalinuia kujibu maswali manne:

1. Kwa kuzingatia vikoa maana, ni maneno mkopo yapi ya Kikamba kutoka Kiswahili yanayojitokeza?
2. Ni kanuni zipi zilizoongoza utohozi maana wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili?
3. Maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yanadhihirisha athari zozote katika mfumo leksia?

### 1.4 Tahadhania za Utafiti

1. Zipo kanuni ambazo huelekeza taratibu za utohozi maana.
2. Maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yameathiri mfumo asili wa kileksia.

### 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Mada ya maneno mkopo inaweza kushughulikiwa kuegemea taaluma tofauti hasa fonolojia, mofolojia au semantiki. Kimsingi, utafiti wetu ulilenga utohozi maana; viwango vya fonolojia na mofolojia havikuchunguzwa moja kwa moja isipokuwa pale ambapo vilidhamiriwa kuchangia uchanganuzi semantiki.

Vipengele msingi vya uchanganuzi semantiki ni vinne: kanuni bia za utohozi maana, taratibu za utohozi maana, athari za utohozi semantiki na etimolojia (Taz Anttila 1972,

Crowley 1997 na Bynon 1977). Kazi hii ililenga kanuni za utohozi maana. Aidha taratibu za utohozi maana na athari za maneno mkopo zilipitiwa kwa lengo la kushadidia kiini cha utafiti huku kipengele cha etimolojia kikiepukwa. Vipengele vilivyolengwa vina uhusiano wa karibu wa kiisimu na kuingiliana katika utaratibu wa uchanganuzi.

Kanuni za utohozi semantiki ni swala ambalo limezuliwa na Anttila (1972). Mwanaisimu huyu anaelezea kuwa kuna mielekeo bia ya michakato ya kisemantiki. Kanuni bia za utohozi maana ni vigezo ambavyo huelekeza maana za maneno mkopo aidha kuchukua mkondo wa maana kupanuka au kufinyika. Umuhimu wa mawasiliano katika muktadha wa kitamaduni huchukuliwa muhimu kwenye uchanganuzi wa kanuni husika. Utafiti huu ulibainisha na kujadili kanuni za kiisimu, kijamii na kihistoria.

Taratibu za utohozi maana ni njia au mbinu zinazotumiwa kutohoa maana. Wataalamu wamefafanua kuwa baadhi ya maneno mkopo hubadili maana awali bila kugeuza umbo la neno (Taz Anttila 1972 na Mwihaki 2006). Taratibu za utohozi maana katika kazi hii zimejadiliwa kwa lengo la kufafanua zaidi jinsi kanuni za utohozi maana huelekeza taratibu za utohozi maana. Utafiti huu ulijadili taratibu nne kutegemea data nyanjani: ufinyizi, upanukaji, usogezi na urari.

Mfumo wa leksia ulitubidi kutalii athari za maneno mkopo katika matumizi ya lugha ya mzungumzaji asili wa lugha ya Kikamba. Aidha swala la vikoa maana na ualama limeguziwa katika kazi hii kwa lengo la kubainisha athari za kimuundo zilizosababishwa

na maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Maneno mkopo huchukua nafasi tofauti katika vikoa maana kutegemea sababu za ukopaji wa neno hilo. Nafasi iliyochukuliwa na neno mkopo huathiri ualama. Uteuzi wa mada ulijikita katika misingi ifuatayo.

**1.6 Sababu za Kuchagua Mada**

Aidha tawi la semantiki halijakua kufikia kiwango cha matawi mengine ya isimu kama vile fonolojia, mofolojia na sintaksia. Jambo hili limezua msisimko mkubwa miongoni mwa wanaisimu kuanzia karne ya ishirini. Kwa mujibu wa msingi huo, utafiti huu ulilenga kuchangia taaluma ya semantiki kwa jumla hasa semantiki ya maneno mkopo.

Utafiti huu ulilenga kutumikiza nadharia ya isimujamii na sarufi kutalii maswala ya isimu linganishi historia. Kwa kufanya hivyo, kazi hii ilitoa nafasi ya kushawishi maeneo mengine hasa katika nyanja za kanuni na matokeo ya mtagusano wa lugha. Utumikizi wa nadhari hizi pia ulilenga kuonyesha nadharia hazina mpaka tunapozingatia nyanja tofauti za lugha. Aidha nadharia hizi zimechangia uchanganuzi wa data katika kazi hii ya semantiki tawi ambalo limekwepwa kwa sababu za kinadharia.

Dhana ya maana huaminiwa kuwa dhahania. Sababu hii ni miongoni mwa sababu zinazowakwaza wanaisimu. Kwa kuzingatia maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili, utafiti huu ulilenga kuweka wazi dhana ya maana na mahusiano ya



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kisemantiki. Imebainika kuwa, utafiti huu ulilenga kueleza kwa kina utohozi maana na hivyo kuchangia weledi wa mfumo wa maana leksia.

Uchanganuzi wa utohozi maana umeonekana kusawiri mifanyiko mingine kama vile fonolojia na mofolojia japo si moja kwa moja. Data ya utafiti huu, hueanda ikachangia katika usomi wa utohozi fonolojia na utohozi mofolojia.

Ukopaji ni dhana ambayo huingiliana sana na mabadiliko ya lugha hasa tunapozingatia ualama na vikoa maana. Katika misingi hiyo, maneno mkopo yanaweza kutumika kudokeza umbo awali la neno na hivyo kuchangia kutalii mabadiliko ya fonolojia, mofolojia na pia semantiki. Data tuliyokusanywa huenda ikafaa katika uchanganuzi wa mabadiliko ya lugha ya Kikamba katika nyanja mbalimbali.

Maneno mkopo katika mawanda ya vyakula, mavazi, vifaa vya nyumbani, teknolojia, dini, wanyama wafugwao, siasa na maisha kwa jumla tuliyokusanya ni dhihirisho la tukio la kihistoria kama vile mtagusano wa utamaduni. Mtagusano huu ulisababishwa na biashara na matukio mengine ya kijamii. Maneno mkopo katika mawanda ya maana ni kifaa muhimu kwa anthropolojia na historia kwani maneno hayo hudhihirisha mtagusano wa tamaduni. Matokeo ya utafiti huu huenda yakafaa wanahistoria na wanaanthropolojia kwa marejeleo yao.

Lugha ya Kikamba ni miongoni mwa lugha za Kibantu zilizosambaa kote Afrika ya Mashariki, Kati na Kusini. Utafiti huu basi ni wakilisho mwafaka kwa lugha za Kibantu. Aidha kazi hii imelenga kuchangia maendeleo ya isimu ya lugha za Afrika hasa lugha ya Kikamba.

### 1.7.0 Tahakiki ya Maandishi

Maandishi yaliyopitiwa yalidhihirisha ukopaji wa maneno ni mojawapo ya sababu za ukuaji wa lugha. Vitu vyote duniani hukua na vivyo hivyo lugha (Taz. Anttila 1972). Miongoni mwa nyanja za lugha ambazo hudhihirisha ukuaji ni pamoja na; fonolojia, mofolojia, kanuni za kisintaktiki, sarufi na semantiki. Kulingana na mahusiano haya, tahakiki ya maandishi ilitambua maeneo matatu muhimu: ukuaji wa lugha, ukopaji na utohozi wa maneno mkopo.

### 1.7.1 Maandishi kwa Ujumla Kuhusu Ukopaji

Waandishi mbalimbali wa isimu linganishi historia na isimu historia wamefafanua dhana ya ukopaji (Taz. Hockett 1958, Anttila 1972, Bynon 1977, Lyons 1992, Mc Mahon 1996, Crowley 1997 na Campbell 1998). Ukopaji ni ule mchakato wa kuhamisha kipashio kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine.

Maandishi haya pia yameelezea sababu za ukopaji kama ukosefu wa istilahi, maingiliano marefu ya kitamaduni, utabaka na kasumba za uzungumzaji. Aidha maandishi mengi yanasisitiza sababu ya ukopaji ni uhitaji na utabaka. Inabainika kuwa, mtagusano wa

Kikamba na Kiswahili umesababisha ukopaji kwani umechukua zaidi ya karne moja (Taz Ogoti 1976). Jambo muhimu kwa mwanaisimu anayetalii maswala ya maneno mkopo ni jinsi ya kutambua maneno hayo miongoni mwa maneno asili ya lugha husika.

Vigezo vya kutambua maneno mkopo vimeshughulikiwa na waandishi wengi hasa Campbell (1998). Maandishi haya yanaangazia vigezo vitano. Dalili za kifonolojia ni mojawapo ya vigezo vya kutambua maneno mkopo. Maneno yaliyokopwa hudhihirisha mwambatano wa sauti ambao si wa kawaida. Kigezo kingine ni muundo wa kimofolojia. Muundo mgeni utasawiri mkondo wa ukopaji. Kigezo cha tatu ni maana mnasaba. Iwapo maneno ni sawa kimuundo na maana, basi lugha hizo zahusiana kiukoo na iwapo hazihusiani, basi moja imekopa. Dalili za kijiografia ni kigezo kingine. Kigezo hiki huangazia maneno ambayo yanarejelea vifaa ambavyo awali havikupatikana eneo husika. Kwa mfano, katika lugha ya Kikamba, neno *mũnathi* 'mnazi' hutumika kurejelea mmea ambao haukupatikana eneo la Ukambani awali bali mwambao wa pwani. Kigezo cha mwisho ni dalili za kisemantiki. Wakati mwingine mahusiano ya kisemantiki hudhihirisha maneno mkopo. Baadhi ya vigezo hivi, vilitumika kutambua maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili.

Waandishi wameonyesha kuwa kuna mbinu tatu za ukopaji: tafsiri, utohozi na sisisi (Taz Bynon 1977 na Campbell 1998). Katika mbinu ya tafsiri, lugha pokezi hutafsiri vifungu vya lugha changizi vinavyokopwa. Kupitia utohozi, maneno kutoka lugha changizi hunukuliwa kwa kuzingatia mfumo wa kiisimu wa lugha pokezi. Kukopa sisisi ni ukopaji

wa moja kwa moja; mbinu hii huchukua maneno jinsi yalivyo katika lugha changizi na kuyatumia hivyo katika lugha pokezi. Utafiti wetu ulidhamiria kulenga utohozi kwa hivyo, usomi zaidi ulilenga dhana ya utohozi.

### 1.7.2 Maandishi ya Jumla Kuhusu Utohozi

Hapo awali tulitaja kuwa utohozi ni mchakato wa kubadilisha maneno ili yaafiki masharti ya lugha pokezi. Utohozi wa lugha hutokea viwango vyote vya lugha: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Utohozi katika kiwango cha fonolojia uhusisha sauti kupitia kanuni za kifonolojia za lugha kopaji ili kuafiki mfumo sauti wa lugha pokezi. Nao utohozi wa mofolojia na sintaksia uhusisha maneno mkopo kupitia kanuni za sintaktiki ili yatoholeke. Miongoni mwa maandishi tuliyotaja, ni machache yaliyojadili utohozi viwango vyote vinne. Utohozi wa fonolojia na mofolojia umejadiliwa kwa kina huku utohozi maana ukinguziwa tu (Taz Hocket 1958, Lehmann 1962, Anttila 1972, Bynon 1977, Mcmahon 1994 na Lyle 1998). Hata hivyo, maandishi yaliyojadili utohozi maana yameweka mambo ya kimsingi wazi: utaratibu wa utohozi maana, kanuni bia za utohozi maana na athari za utohozi maana. Utohozi maana hutumia taratibu sita maalum; upanuzi maana, ufinyizi maana, uimarikaji maana, udhalilikaji maana, tasfida na usogezi maana.

Upanuzi maana hutokea pale ambapo maana za nomino hupanuka ili kutumika katika miktadha mingi ya mawasiliano kuliko awali. Ufinyizi maana nao huwa kinyume cha upanuzi; miktadha ya neno katika matumizi hupunguka. Uimarikaji maana hutokea pale

ambapo maneno yaliyokataliwa na jamii kwa sababu za kitamaduni hukubalika na neno likatumika. Haya hutokea kupitia mabadiliko ya kisaikolojia au mpito wa wakati. Udhalilikaji maana nao ni kinyume cha uimarikaji; kudhoofika kwa maana ya maneno kwa sababu za kitamaduni. Aidha kutaja maneno haya huwa ni mwiko. Kila jamii huwa na vigezo vya tamaduni na miiko ambayo huelekeza na kuendesha mazungumzo. Baadhi ya matamshi hukatazwa na kuwekewa vikwazo. Vigezo hivi vya kitamaduni katika mawasiliano ni tasfida. Utaratibu wa usogezi maana hutokea pale ambapo maana ya neno husogezwa katika lugha pokezi. Mbinu kadha hutumika kufafanua usogezi maana: istiari, metonimu na sinedochi. Istiari hutumika kuonyesha uhusiano wa kimaana kwa mujibu wa matumizi yake huku metonimu ikifafanua mabadiliko ya maana ya neno inapopanuka na kuhusisha maana zingine. Sinedochi ni pale ambapo sehemu ndogo ya dhana hutumika kuwakilisha sehemu kubwa.

Maandishi awali kuhusu utohozi maana yaliupa utafiti wetu msingi na mwangaza wa utafiti zaidi. Kulingana na maandishi awali, kuna uwezekano wa kutalii jinsi maneno mkopo yanavyoathiri mahusiano ya kisemantiki awali ya lugha pokezi. Aidha, kanuni bia zinazoelekeza maana ya maneno mkopo kupanuka au kufinyika ziliweza kuchunguzwa. Katika misingi hii, maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yalichanganuliwa. Ikumbukwe kuwa, lugha ya Kikamba ni miongoni mwa lugha za Kibantu na hivyo maandishi yoyote yanayolenga utohozi katika lugha za Kibantu yalichangia utafiti wetu.

### 1.7.3 Maandishi ya Jumla Kuhusu Utohozi Katika Lugha za Kibantu

Usomi wa awaliulibainisha kuwa, kuna maandishi machache yanayolenga utohozi katika lugha za Kibantu. Maandishi ya Whiteley (1963) yanalenga utohozi wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili na Kiingereza. Mambo muhimu katika utafiti wetu yanadokezwa na maandishi haya. Jamii ya Wakamba imeingiliana na watu wa mwambao wa pwani kwa miaka mingi kwa minajili ya mahitaji ya uchumi. Lugha ya Kikamba imekopa kutoka lugha ya Kiswahili kwa sababu za kuelezea dhana geni na pia teknolojia mpya. Whiteley (ibidi) anakubaliana na wataalamu wengine kuwa ukopaji huchukua mbinu tatu naye anachanganua mbinu ya utohozi. Uchanganuzi wake unalenga utohozi viwango vitatu vya lugha: fonolojia, mofolojia na semantiki. Maandishi haya, yalidokeza kuwa japokuwa utafiti wa maneno mkopo huegemea isimu linganishi historia, ni sharti muktadha wa kijamii utiliwe maanani wakati wa utafiti. Aidha mtazamo huu ulilazimu utafiti wetu kuangazia maswala ya isimujamii japokuwa si moja kwa moja.

Maandishi yaliyopitiwa pia yalidokeza kuwa maana ya maneno mkopo yanaweza kutazamwa kwa kuegemea mikondo mitatu: maana ya maneno mkopo yakilinganishwa na maana katika lugha changizi, maana ya maneno mkopo yakilinganishwa na maana awali lakini maana ikiwa imepanuka na maana ya maneno mkopo pasipo kutilia maanani maana awali. Mikondo miwili ya kwanza ilifaa utafiti wetu katika kutalii taratibu za utohozi maana. Aidha maandishi haya yalibainisha uchanganuzi wa utohozi maana kutofanyika kiwango cha kuridhisha kwa sababu mbili: kwanza, ukosefu wa data ya kutosha kuangazia muktadha uliohitajika kwa maana kamili na; pili, utata wa kanuni za

utohozi semantiki. Kutokana na maandishi haya, utafiti wetu ulionekana kuwa na nafasi ya kutafitia zaidi swala la maana za maneno mkopo ya Kikamba.

Maneno mkopo ya Kiswahili pia yametazamwa kwa lengo la kubaini kiini cha ukopaji (Taz. Whiteley 1963, na Mbaabu 1985). Uchunguzi huu haujajishughulisha na mifanyiko ya maneno mkopo ili kuafiki mfumo wa lugha pokezi. Maandishi haya yameonyesha dhana ya ukopaji wa maneno bila kuangazia ndani mifanyiko ya fonolojia, mofolojia na semantiki. Maandishi ya Whiteley na Muli (1962) yanadhihirisha kuwa lugha ya Kikamba imekopa zaidi kutoka lugha ya Kiswahili.

Kwa jumla, maandishi kuhusu utohozi katika lugha za Kibantu yatachukuliwa kama nanga katika utafiti wetu hasa kazi ya Whiteley (1963). Maandishi haya pia yamedokeza changamoto katika kutalii kanuni bia za utohozi maana huku yakipendekeza muktadha mpana wa kijamii. Aidha mapendekezo ya maandishi awali yalitufaa katika uteuzi wa nadharia ya utafiti. Baadhi ya data kutokana na maandishi awali ilitumika katika uchanganuzi wetu. Mbali na maandishi, zipo tafiti bayana ambazo zinatalii maswala ya utohozi.

### 1.7.4 Tafiti Bayana Kuhusu Utohozi Katika Lugha za Kibantu

Tafiti nyingi zimelenga utohozi wa kifonolojia na kimofolojia. Mwihaki (1998) alichunguza utohozi wa maneno mkopo kiwango cha kifonolojia lugha ya Gikuyu. Utafiti huo ulichanganua taratibu za utohozi wa kifonolojia. Ngesu (2005) ametafitia

usimilisho wa kifonolojia na kimofolojia katika maneno mkopo ya Kikamba lahaja ya Mwingi kutoka Kitharaka na Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalionyesha asilimia kubwa ya maneno mkopo ya Kikamba ni kutoka Kiswahili.

Utafiti uliochanganua misingi ya semantiki uliegemea taratibu za utohozi katika maneno ya Sheng` (Taz. Mugambi 2007). Kimsingi utafiti huo ulifafanua mfumo wa leksia katika Sheng' na kuepuka kanuni za utohozi wa kisemantiki. Lugha ya Sheng' twafahamu ilizuka kutokana na lugha zingine za Kiafrika. Tunaweza kudai kuwa lugha ya Sheng' haina muundo msingi asili ila imekopa (Taz Mbaabu 2003). Tukizingatia mtazamo huo, lugha ya Sheng' haina muundo leksia asili ambao waweza kutazamwa kuathiriwa na maneno mkopo. Mjadala huu uliipa kazi yetu nafasi ya kutalii lugha ya Kikamba ambayo ni miongoni mwa lugha asili za Kibantu yenye miundo msingi. Utafiti wetu ulionekana kuwa na nafasi bora zaidi katika kutalii athari za maneno mkopo ya Kiswahili katika muundo asili wa kisemantiki wa lugha ya Kikamba. Aidha kazi ya Mugambi (ibidi) imechangia utafiti wetu katika eneo la taratibu za utohozi maana.

Tafiti awali zilizopitiwa zilionekana kuweka msingi na kutoa nafasi ya utafiti wetu. Kazi husika pia zilisisitiza umuhimu wa swala la kijamii na tamaduni katika kutalii maana. Katika misingi hiyo, utafiti wetu ulibidika kutilia maanani muktadha mpana wa kitamaduni na kijamii unaozunguka maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Mtazamo huo ulielekeza utafiti wetu kutumikiza nadharia ambazo uchanganuzi wake wa lugha huegemezwa katika vigezo vya kitamaduni na vigezo vya kijamii.

### 1.8.0 Misingi ya Kinadharia

Nanga ya utafiti wetu ni kanuni za utohozi semantiki. Tulidokeza kanuni hizi huelekezwa na vipengele vya kiisimu, kijamii, kihistoria na saikolojia. utafiti wetu pia uliegemea isimu linganishi historia (Taz Usuli wa Mada). Mwelekeo wa utafiti wetu uliibua maswala mawili muhimu: uchanganuzi wa lugha katika misingi ya jamii na uchanganuzi wa lugha katika misingi ya mawasiliano. Misingi hiyo ilielekeza kazi yetu kuchukua mtazamo changamano wa kinadharia. Nadharia ya Tahakiki Usemi, ikishirikiana na Sarufi Amilifu Mfumo iliteuliwa.

### 1.8.1 Tahakiki Usemi

Tahakiki Usemi (TU) ni nadharia inayoangazia maswala ya isimujamii. Isimujamii huchunguza lugha katika muktadha wa kijamii. Kutokana na isimujamii, uhusiano wa lugha na jamii hudhihirishwa. Nadharia ya TU ilianzishwa na Norman Fairclough (1989) alipohisi ya kwamba nadharia awali za isimujamii zilipungukiwa katika kutalii maswala ya isimujamii. Fairclough (ibidi) alitaka kuchanganua lugha kwa lengo la kuonyesha jinsi lugha inavyosababisha utabaka miongoni mwa wanajamii. Tahakiki Usemi hutazama lugha kama kifaa muhimu katika shughuli za kijamii. Lengo la nadharia hii ni kuonyesha mahusiano miongoni mwa wanajamii kama vile mahusiano ya lugha, utabaka na itikadi huku itikadi ikichukuliwa kuwa kipengele muhimu sana katika mawasiliano ya wanajamii. Katika hali ya kuelewa mahusiano ya lugha, utabaka, itikadi na mchakato wa tafsiri ni muhimu. Mchakato huu hujumuisha umbo la usemi na viwakilishi dhana tofauti akilini. Viwakilishi dhana husawiri muktadha mpana wa vitu kama umbo la maneno,

muundo wa sentensi na mpangilio wa matukio katika muktadha maalumu. Baadhi ya viwakilishi dhana ni vya kiisimu na baadhi si vya kiisimu.

Tahakiki Usemi pia, hutazama lugha kama usemi; lugha ni mfumo wa uzoevu wa kijamii. Lugha kama uzoevu wa jamii, ni wazo ambalo linazua mambo matatu muhimu: lugha na jamii hufungamana; lugha ni mchakato wa kijamii na; lugha ni mchakato wa uzoevu wa kijamii. Lugha kama sehemu ya jamii, ni kumaanisha matukio yote ya kiisimu ni ya kijamii; wanajamii wanapozungumza, kusikiliza, kuandika au kusoma hufanya hivyo katika miktadha ya kijamii. Kwa jumla, lugha hutumika kudumisha mahusiano ya kijamii. Lugha inapochukuliwa kama mchakato wa kijamii, michakato ambayo hudhihirika katika usemi huangaziwa. Usemi hutumika kurejelea mchakato jumulifu wa kijamii ambapo matini ni sehemu yake. Katika uchanganuzi wa usemi, kuna michakato mitatu: mahusiano, uzalishaji (ambapo matini ni zao) na utafsiri (ambapo matini ni chumo). Nayo matini ni kiwakilishi cha lugha aidha iliyoandikwa au iliyozungumzwa; matini ni namna yoyote ya lugha ambayo yaleta maana kwa mweledi wa lugha hiyo (Taz Fairclough 1989 na Halliday 2004). Kwa hivyo matini ni zao wala si mchakato. Uchanganuzi wa matini ni sehemu ya uchanganuzi wa usemi. Hata hivyo, hakuna mchakato wa uzalishaji na utafsiri unaoweza kukamilika bila kutilia maanani jinsi mchakato huo unavyoathiriwa na maswala ya kijamii. Mtazamo huu, ulimfanya mhasisi wa nadharia hii kuiona lugha kama uzoevu wa kijamii.

Lugha kama uzoevu wa kijamii humaanisha kuwa lugha imedhibitiwa na vikwazo vya kijamii visivyokuwa vya kiisimu; aidha baadhi ya vikwazo vinavyoathiri lugha ni vya kijamii wala si vya kiisimu. Viwakilishi dhana ambavyo wanajamii hutumia kuzalisha na kutafsiri matini vimo akilini mwa wanajamii lakini chimbuko lake ni jamii. Kwa hivyo, umbo la viwakilishi dhana hutegemea muktadha mpana wa kijamii (mahusiano ya kijamii na vikwazo vya kijamii) ambapo vimezalishwa na kutafsiriwa. Kwa hivyo mfumo wa lugha ni sehemu ya mfumo wa jamii. Ni sawa kusema, wanajamii hutafakari yaliyozalishwa na jamii na kutumia tafakari hizo katika shughuli za kijamii ukiwemo usemi. Mawazo haya yote yanaoana kuleta maana kuwa, usemi uhusisha vikwazo vya kijamii kwa namna mbili; vikwazo vya kijamii katika uzalishaji wa matini na vikwazo vya kijamii katika utafsiri wa matini. Vikwazo hivi vya kijamii vinahusiana na viwango vitatu vya utaratibu wa kijamii; muktadha wa kijamii ambao usemi hutokea, kiwango cha asasi za kijamii ambazo uhusisha muktadha mpana wa usemi na kiwango cha jamii jumulifu. Vikwazo hivi vya kijamii huvipa viwakilishi dhana umbo ambalo wanajamii hutumia kuzalisha na kutafsiri matini. Mtazamo huu umewezesha utafiti wetu kutalii tafsiri mbalimbali zilizopewa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili na jamii ya Wakamba.


Aidha tulidokeza kuwa, uchanganuzi wa matini ni sehemu ya uchanganuzi wa usemi kumaanisha michakato ya uchanganuzi ni sawa. Mtafiti anayehakiki matini ni sharti azingatie mchakato wa uzalishaji, utafsiri, mahusiano ya matini, vikwazo vya kijamii ambavyo vinalenga hali, asasi na miundo ya jamii husika. Kwa kifupi, ni sharti uhusiano



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kati ya matini, mahusiano yenyewe na muktadha kutiliwa maanani; kuzalishwa kwa matini hudhibitiwa na vikwazo vya kijamii vya uzalishaji matini na utafsiri matini. Vikwazo hivi vinahusiana na viwango vitatu vya utaratibu wa kijamii: muktadha wa mawasiliano, kiwango cha asasi za kijamii ambazo hujumuisha mawazo pana ya usemi na kiwango cha jamii jumulifu. Leksimu zilizokusanywa nyanjani maana zake zimehafikiwa kwa kuzingatia mchakato wa uzalishaji na utafsiri matini. Tazama mchoro ufuatao:

**(1.1) Usemi kama Matini, Mahusiano na Muktadha**



Mwelekeo wa TU katika uchanganuzi wa lugha, unatambua hatua tatu muhimu. Hatua hizi huelekeza uchanganuzi wa lugha kwa uangavu zaidi huku matini ikichukuliwa kama nanga ya matumizi ya lugha. Labda tueleze kuwa, maana ya maneno haijitokezi kikamilifu bila kuzingatia matumizi ya maneno hayo katika sentensi. Kwa mtazamo huo, hatua zinazopendekezwa na TU zilitumika kama mihimili katika utafiti wetu. Hatua za uchanganuzi:

1. Maelezo- Hushughulikia zile milki za matini.
2. Fasiri - kufasiri mahusiano ya matini kama zao la mchakato wa uzalishaji na matini kama chumo la mchakato wa tafsiri
3. Fasili - kufasili uhusiano kati ya mahusiano na muktadha wa kijamii.

Nadharia ya TU hupendekeza matumizi ya nadharia ya kisarufi hasa katika uchanganuzi wa sarufi. Japokuwa nadharia yenyewe ni ya isimujamii, nanga yake ni lugha ambayo haina budi kuchanganuliwa kwa kuegemea vigezo vya kisarufi. Pili, kwa madhumuni ya uchanganuzi wa lugha, dhana ya umilisi mawasiliano ni muhimu. Kwa kukidhia mahitaji hayo nadharia ya TU tuliteua nadharia ya kisarufi ambayo itashughulikia swala la mfumo lugha kwa uangavu ambayo ni Sarufi Amilishi Mfumo.

### 1.8.2 Sarufi Amilishi Mifumo

Sarufi Amilishi Mfumo (SAM) kwa mujibu wa Halliday (1985, 1994 na 2004) hutazama lugha kama mtandaa wa maana ambao huwakilishwa kwa matini za kisarufi. Lugha huonekana sawa na sheria za kisarufi zinazoshirikiana na ujuzi wa mahusiano ya kijamii. Sarufi Amilishi Mfumo imetambua na kufuma tanzu tatu za sarufi: sintaksia, semantiki na pragmatiki.

1. Semantiki - ni uhusiano kati ya maumbo na maana msingi
2. Pragmatiki - ni uhusiano wa maana na msemaji kulingana na muktadha wa matumizi ya lugha
3. Sintaksia - ni uhusiano kati ya maumbo lugha yenyewe.

Sarufi Amilishi Mfumo inatazama matini kwa namna ambavyo inakidhi mahitaji ya umilisi mawasiliano na utoshelevu wa kipragmatiki. Lugha ni ishara ya kipragmatiki, ishara ya kufanikisha mawasiliano, pale ambapo pragmatiki hudhibiti semantiki nayo semantiki ikaja kudhibiti sintaksia. Kwa mujibu wa mahusiano haya, lugha haieleweki vya kutosha iwapo maswala ya kipragmatiki yatapuuzwa. Kwa juhudi za kukidhi mahitaji haya, Sarufi Amilishi Mfumo imetambua aina tatu za maana: maana dhanishi, maana tagusani na maana matinishi.

Maana dhanishi pia huitwa maana tambuzi na ni kitengo cha maana ambacho huwakilisha uwezo wa msemaji wa kutambua mambo. Maana hii kwa hivyo ndiyo

hubeba maudhui katika lugha. Kupitia maana dhanishi, lugha husimba tajiriba za kitamaduni na kijamii naye msemaji akisimba tajiriba zake binafsi. Ni kupitia maana dhanishi ambamo tunatwaa ujuzi na weledi wa ulimwengu tunamoishi, na pia kuwasilisha tajiriba zetu. Hivi ni kusema kwamba maana dhanishi humilikiwa kama nyenzo ya kuelewa na kueleza ujuzi na tajiriba kwa jumla.

Maana tagusani ni maana jamilishi, na kwa jumla, maana husishi. Inasimamia kitengo tangamanishi cha matumizi ya lugha kuegemea vikwazo vya kijamii. Maana tagusani inawafaa wasemaji wa lugha kama nyenzo ya kufasili na kutafsiri wajibu na dhima ya kijamii. Kupitia maana tagusani wasemaji wanatumia lugha kwa minajili ya kuasisi, kuimarisha, na kudumisha masharti ya mahusiano ya kijamii. Matumizi ya maana tagusani yanategemea dhima na mahusiano ya kijamii.

Maana tagusani inabainika kama amali tekelezi ya lugha. Amali tekelezi inazingatia matumizi lugha kama tendo la usemi. Msemaji ni mtenda, ambaye hujiingiza katika tendo hilo. Hivi ni kusema msemaji ni mshirika wa tendo la usemi, kwa namna ambavyo anajiingiza katika muktadha na hali halisi ya mawasiliano, ili aweze kujieleza na kuelewa. Msemaji anaeleweka kwa kugusa mielekeo, imani, tabia, falsafa, hisia, pamoja na mawazo ya msikilizaji. Mtagusano kimawazo utahitaji mantiki ya maana dhanishi.

Kwa pamoja maana dhanishi na maana tagusani hushirikisha kanuni bia za matumizi ya lugha, ambayo ni kudhibiti mazingira yetu maishani na kutumia akili zetu. Kulingana na

madai haya, kila lugha ulimwenguni imeundwa kwa maana mbili za kimsingi: maana dhanishi na maana tagusani. Maana dhanishi kwa upande wake inasimamia dhati ya ujumbe, nayo maana tagusani inatazama kaida za vikwazo jumulifu vya kimawasiliano na kijamii. Hizi basi ndizo amali za kimsingi, hata hivyo, uwasilishi wa dhima mbili za kimsingi utategemea amali ya tatu: maana matinishi.

Maana matinishi inarejelea jumla ya kanuni za sarufi na ufasaha wa mawasiliano ya lugha. Hivi ni kusema kwamba maana matinishi inaelekeza matumizi ya lugha; inampatia msemaji vifaa vya kuwasilisha ujumbe kwa njia yenye usarifu na ufasaha kulingana na vikwazo vya muktadha na hali ya mawasiliano. Hapo basi maana matinishi inaingiza muwala katika matumizi ya lugha. Muwala unabainika kupitia uwiano baina ya matumizi ya kisarufi na mahitaji ya mazingira ya mawasiliano.

Hivi ni kusema kwamba maana matinishi inatekeleza jukumu la uwasilishi. Lakini itakuwa ni kupitia ushirikiano na maana dhanishi kwa upande mmoja, na maana tagusani kwa upande mwingine, ambamo maana matinishi itafanikiwa kwa kuwakilisha ujumbe kwa namna ambavyo ulidhamiriwa. Matini ndogo zaidi ambayo hutumika kama msingi wa uchanganuzi ni kishazi.

Kisahazi hicho kimenasibishwa na sentensi sahili na kina mitazamo mitatu: kishazi kama ujumbe, kishazi kama upokezano, na kishazi kama uwakilisaho.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

1. Kashazi kama ujumbe ni mtazamo wa kisemantiki unaolingana na amali maana dhanishi.
2. Kishazi kama upokezano ni mtazamo wa kipragmatiki unaolingana na amali maana tagusani.
3. Kisahazi kama uwakilishi ni mtazamo wa kisintaksia unaolingana na maana manishi.

Mahusiano haya yanaashiria kuwa, kuna uwiano kati ya tanzu tatu za kisarufi, aina tatu za maana na viwango vitatu vya kishazi. Pamoja na hayo, kuna uwiano baina ya Sarufi Amilishi Mfumo na Tahakiki Usemi. Nadharia zote mbili zinasisitiza nafasi ya muktadha wa kitamaduni na muktadha wa mawasiliano katika kutalii matumizi ya lugha. Bora zaidi mwelekeo wa nadharia hizi ulielekeza mbinu za utafiti.

**1.9.0 Mbinu za Utafiti**

Uchunguzi wetu ulihusisha mbinu mbili kuu za uchunguzi: utafiti wa maktabani na ule wa nyanjani. Utafiti wa maktabani ulizingatia maswala kuhusu mtagusano wa lugha, ukopaji wa lugha na hasa utohozi wa maneno mkopo huku uzito ukitiliwa utohozi maana. Vitabu, makala, tasnifu, majarida na machapisho yanayohusiana na mada ya utafiti yalipitiwa. Mtandao ulikuwa wa msaada hasa kwa makala ya hivi karibuni yanayolenga utohozi maana.

Utafiti msingi zaidi ulielekea nyanjani kwa lengo la kukusanya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili ili yachanganuliwe kimaana. Kimsingi, utafiti wa nyanjani ulihusisha hatua tatu kuu: mbinu za kubainisha na kukusanya data, mbinu za kuchanganua data na mbinu za kuwasilisha data.

### 1.9.1 Mbinu za Kukusanya Data

Ukusanyaji wa data ulihitaji kutilia maanani mambo manne: eneo la ukusanyaji data, mbinu za kutambua maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili, mawanda yatakayolengwa, uteuzi wa sampuli na utaratibu wa kukusanya data. Maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yalitambuliwa kwa kufuata vipengele vilivyofafanuliwa katika tahakiki ya maandishi (Taz 1.7.2). vipengele msingi ni: dalili za kifonolojia, muundo wa kimofolojia, na dalili za kijiografia.

Ukaguzi wa awali ulidhihirisha maeneo ya Kitui Kati, na Kitui Kusini yanaaminika kuingiliana na watu kutoka mwambao wa Pwani kwa kipindi kirefu ambao walitumia lugha ya Kiswahili kama chombo cha mawasiliano. Kwa misingi hii, utafiti huu ulilenga kukusanya data maeneo haya.

Tulitanguliza kusema kuwa maneno hujitokeza katika mafungu yenye uhusiano wa kimaana (Taz Cruse 2000). Mafungu haya hudhihirisha mawanda maalumu aidha kurejelea teknolojia, sanaa na mahusiano ya kijamii miongoni mwa mengine. Sababu hii ilielekeza ukusanyaji wa data kulenga mawanda yaliyoangazia maswala ya jamii.

Mawanda haya ni kama jamii, dini, elimu, afya, mavazi, usafiri, zaraa, uchumi na vifaa vya jikoni. Data kutoka mawanda haya imesaidia uchanganuzi wa vikoa maana.

Kanuni zilizopendekezwa na Kibrik (1977) zilifuatiliwa katika ukusanyaji wa maneno mkopo. Kanuni ya kwanza ni uzoevu wa neno; maneno mkopo yaliyoonekana kujitokeza katika miktadha mbalimbali yalikusanywa. Kanuni ya pili ni maneno ambayo ni mwangwi wa utamaduni wa lugha changizi na inajikita katika ukweli kuwa maneno huwa polisemia na gombo la maana ya maneno hutofautiana katika lugha tofauti. Kigezo hiki kilielekeza kiasi cha maneno mkopo yaliyokusanywa, ambayo yanarejelea vifaa halisi ulimwengu halisi kutokana na lugha changizi. Kanuni ya tatu ni ule ukubalifu wa kisintaksia wa maneno ambao uliwezesha kulenga maneno yanayopatikana katika vikoa maana.

Mahojiano, mijadala na njia ya mshiriki mkaguzi ni mojawapo ya mbinu zilizotumika kukusanya data. Uteuzi wa wahojiwa ulitegemea sampuli yakini ambapo vigezo vya kipragmatiki kama vile umri, jinsia na hadhi vilizingatiwa kwani vigezo hivyo husaidia kuwasilisha ujumbe kwa njia inayokubalika. Wahojiwa wenye umri wa miaka kuanzia sabini kwenda juu waliteuliwa kwa sababu ya tajiriba na uzoevu wao wa lugha. Umilisi wa lugha zote mbili Kikamba na Kiswahili ulikuwa kipengele muhimu kwa kila mhojiwa. Jumla ya wahojiwa thelathini na sita walihojiwa.

Vifaa kama kinasa sauti, kalamu, na daftari, simu ya mkono na vinasa picha vilitumika kukusanya data. Mtafiti alisikiliza na kurekodi maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yanayopendekezwa na wahojiwa. Mtafiti aliwahusisha wahojiwa katika mijadala ya kutambua matumizi mbalimbali ya maneno hayo katika mawasiliano na kurekodi matumizi hayo. Baadaye maneno yaliyorekodiwa yalinakiliwa kwenye daftari kwa kuzingatia mawanda yaliyodokezwa katika mbinu za kukusanya data (Taz 9.1). Baadaye data ilichanganuliwa.

### 1.9.2 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulianza kwa kuainisha maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Utaratibu wa kuainisha data ulizingatia asasi tofauti kama vile elimu, dini au jamii. Uainishaji wa maneno ulisaidia kuyapanga maneno katika makundi ya vikoa maana. Data iliyoainishwa ilichanganuliwa zaidi kwa kuzingatia kipengele cha taratibu za utohozi maana. Aidha taratibu za utohozi maana zilidhihirisha kupanuka au kufinyika kwa fahiwa za leksimu mkopo. Kwa kuzingatia taratibu za utohozi maana kanuni za utohozi maana zimejadiliwa. Swala la athari za maneno mkopo katika muundo asili wa leksika wa lugha ya Kikamba limigisiwa. Uchanganuzi wote umefungamanishwa na kuwasilishwa katika sura moja.

### 1.9.3 Mbinu za Uwasilishaji wa Data

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Taarifa iliyowasilishwa inahusu taratibu za utohozi semantiki, athari za utohozi semantiki katika muundo leksia na kanuni za utohozi maana. Data iliyowasilishwa nanga yake ni jinsi inavyotumika na wazungumzaji asili wa eneo la utafiti. Uwasilishaji huu umejadiliwa katika sura ya tatu.

**Hitimisho**

Sura hii imeweka msingi wa utafiti wetu. Tumejadili mchango wa kazi awali katika utafiti wetu. Tumeonyesha pia nafasi ambayo utafiti huu umelenga kuchangia katika usomi. Katika juhudi za kuuweka wazi uchanganuzi wetu, imetubidi tutalii swala la muundo. Baadhi ya wataalamu wanashikilia msimamo kuwa ni vigumu kuweka mipaka wazi kati ya muundo na maana. Lengo mahususi la muundo ni kufanikisha uwasilishaji wa maana. Ufafanuzi wetu wa muundo katika sura inayofuata unalenga kiwango cha neno kwa lengo la kuweka msingi wa uchanganuzi wa data kutaka nyanjani. Uchanganuzi wa muundo katika kazi hii uchukuliwe kama kiungo cha kufungamanisha utangulizi wetu na uchanganuzi wa kazi yetu.

# SURA YA PILI

# MUUNDO WA MANENO YA KIKAMBA

**Kitangulizi**

Sura iliyotangulia ilidokeza kuwa mfanyiko wa kisemantiki haujisimamii bali una ukuruba wa karibu sana na sarufi (Taz 1.8). Kwanza, kudhihirika kwa leksika katika mawasiliano hudhibitiwa na sheria za kisarufi. Pili, mfanyiko wa kimofolojia kama uundaji wa nomino kutokana na vielezi ni mfanyiko wa uleksikishaji (Taz Anttila 1972 na Cruse 1986). Wazo hili limetubidi kutalii muundo wa maneno ya Kikamba ambayo hutumika kuwasilisha maana. Ufafanuzi wetu umeegemea zaidi data iliyopatikana kutokana na kazi awali kuhusu muundo wa lugha ya Kikamba (Taz Fansworth 1957, Whiteley na Muli 1962, Ford 1975, Maundu 1980, Kitavi 1992, Kimanga 1994 na Kioko 2005). Kwa kawaida, muundo wa maneno huchanganuliwa kupitia viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Ufafanuzi wetu umezingatia viwango vya fonolojia, mofolojia na semantiki.

## 2.1 Muundo wa Kifonolojia

Fonolojia ni utanzu wa sarufi unaochunguza mfumo wa sauti za lugha. Tawi hili hushughulikia jinsi sauti hizi zinavyotumika, zinavyounganishwa, na kupangwa katika lugha yoyote mahsusi ili kuunda tungo zenye maana (Taz Lyons 1981, Anderson 1985, na Odden 2005). Nadharia tulizoteua kuongoza utafiti wetu (TU na SAM), hazikuturuhusu kutalii muundo wa kifonolojia. Ili kufidia upungufu huu, tulibidika kuazima nadharia ya Fonolojia Vitengo Huru (Fonolojia Tenganishi) kwa mujibu wa



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Goldsmith (1990). Fonolojia Tenganishi hutegemea hoja kwamba mfumo wa sauti una mpangilio (rusu) msingi. Kila moja ya vitengo vingine kama vile fonimu, silabi na toni hujitegemea na huwa katika rusu yake yenyewe. Muundo wa kifonolojia kwa hivyo ulichanganuliwa kupitia vigezo vitatu vya kimsingi:

- Fonimu
- Silabi
- Toni

### 2.1.1 Fonimu za Kikamba

Fonimu ni kipashio kidogo kabisa katika lugha chenye kubainisha maana. Fonimu za lugha hutambulishwa kupitia mpangilio wa jozi finyu. Jozi finyu ni maneno mawili yenye maana tofauti lakini yenye kubainisha kupitia sauti moja.

**(2.1) Kielelezo cha Jozi Finyu**

| Fonimu | tahajia | Jozi finyu | tafsiri |
|---|---|---|---|
| /t/ | t | / ta:/ | taa |
| /s/ | s | /sa;/ | saa |
| /a/ | a | /nza/ | nje |
| /e/ | î | /nzî/ | nchi |
| /n/ | n | /una/ | vunja kuni |
| /m/ | m | /uma/ | toka |
| /o/ | û | /îtũ/ | jani |
| /u/ | u | /ître/ | wingu |

Kutokana na mifano yetu, tunaweza kutambua fonimu nane za Kikamba; /t/, /s/, /a/, /î/, /n/, /m/, /ũ/ na /u/. Fonimu hizi zinajumuisha vokali na konsonanti.

### 2.1.2 Vokali za Kikamba

Vokali ni sauti ya lugha inayotamkwa wakati ala za sauti zi wazi kiasi cha kwamba hakuna uzuilifu wa mkondohewa (Taz Yule 1993). Tutatumia jozi finyu kubainisha vokali za Kikamba.

**(2.2) Utambuzi wa Vokali za Kikamba**

| **Fonimu** | **tahajia** | **jozi finyu** | **tafsiri** |
|---|---|---|---|
| /a/ | a | /nza/ | nje |
| / e/ | î | /nzî/ | nchi |
| /ɛ/ | e | /enda/ | enda |
| /i/ | i | /inda/ | bambika |
| / ɔ / | o | /ona/ | ona |
| /u/ | u | /una/ | kuvunja |
| /ũ/ | û | /îtû/ | jani |
| /u/ | u | /îtu/ | wingu |

Jozi finyu hapo juu zadhihirisha kuwa, lugha ya Kikamba ina vokali saba. Vokali hizi zaweza kujitokeza sehemu yoyote katika neno: mwanzo, ndani au mwisho wa neno. Ilivyo kawaida ya lugha kwa jumla, vokali za Kikamba zaweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo vya kawaida vya kifonetiki. Zingatia jedwali lifuatalo.

**(2.3) Jedwali la Vokali za Kikamba**

| Uinuko wa Ulimi | Ulalo wa Ulimi | | |
|---|---|---|---|
| | mbele | kati | Nyuma |
| Juu | i | | U |
| Kati-Juu | e | | O |
| Kati-Chini | ɛ | | ɔ |
| Chini | | a | |

Vokali za Kikamba hudhihirisha maumbo tofauti, ambayo ni vokali sahili, vokali wakaa na vokali changamano. Maumbo tofauti huwakilishwa katika vielelezo matawi. Vokali sahili huwakilishwa kwa kistari kimoja kinachoelekezwa kwenye nafasi moja katika rusu msingi. Maneno *nda* [nda] "tumbo" na *ngi* [ŋgi] "nzi" yanaonyesha vokali sahili, /a/ na /i/

**(2.4) Kielelezo Jedwali cha Vokali Sahili**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu Msingi | V | V |
| | \| | \| |
| Rusu Fonimu | a | i |

Vokali changamano ni mseto wa herufi mbili au zaidi, zenye muundo tofauti zinazotamkwa sawa na kipashio kimoja cha kifonimu. Mifano ya vokali changamano ni /a ɔ/ na /ai/ katika maneno ya silabi moja *ngao* [ŋga ɔ] "ngao" na *ngai* [ŋgai] "Mungu".

**(2.5) Kielelezo Jedwali cha Vokali Changamano**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu Msingi | V | V |
| | /\ | /\ |
| Rusu Fonimu | aɔ | a i |

Wakaa hurejelea urefu wa muda ambao hutumika kutamka fonimu fulani, ukilinganishwa na ule wa kawaida. Vokali wakaa ni mseto wa herufi mbili zenye muundo sawa wa sauti. Kielelezo cha umbo hili huelekezwa rusu msingi kwa vistari viwili. Tazama vokali /a:/ na /i:/ katika maneno ya silabi moja: *ndaa* [nda:] "chawa" na *ngii* [ŋgi:] "mbegu"

**(2.6) Kielelezo Jedwali cha Vokali Wakaa**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu Msingi | vv | vv |
| | \/ | \/ |
| Rusu Fonimu | a: | i: |

Vokali wakaa mara nyingi huashiria tofauti za kileksia. Wakaa wenye dhima ya kileksia pia huitwa wakaa bainifu. Tutadhirisha wakaa bainifu katika vokali zote kupitia jozi finyu.

### (2.7) Wakaa Bainifu

| fonimu | tahajia | unukuzi | tafsiri |
|---|---|---|---|
| /a/ | a | [maka] | shtuka |
| /a:/ | aa | [maka:] | makaa |
| /ɛ/ | e | [mbɛtɛ] | pete |
| /ɛ:/ | ee | [mbɛtɛ:] | niletee |
| /e/ | î | [ende] | lakini |
| /e:/ | îî | [ende:] | lini |
| /i/ | i | [ngi] | nzi |
| /i:/ | ii | [ngi:] | mbegu |
| /ɔ / | o | [ŋgɔ] | chui |
| /ɔ:/ | oo | [ŋgɔ:] | moyo |
| /o/ | û | [ko] | wapi |
| /o:/ | ûû | [ko:] | mguu |
| /u/ | u | [ču] | hicho |
| /u:/ | uu | [ču:] | kivuli |

Dhana ya wakaa huashiria kwamba muda wa kutamka sauti moja hupimika. Kipimo kidogo zaidi cha muda wa matamshi huitwa mora. Vokali wakaa ina mora mbili na kwa hivyo pia huitwa sauti ndefu. Kwa pamoja vokali sahili na vokali changamano ni sauti fupi kwa sababu zinalinganishwa na muda wa mora moja. Dhana ya umbo la fonimu itarejelewa tena kuhusiana na konsonanti za Kikamba.

### 2.1.3 Konsonanti za Kikamba

Konsonanti ni sauti ambazo zinapotamkwa mkondohewa huzuiliwa aidha kooni au kinywani. Tutatumia jozi finyu kubainisha konsonanti za Lugha ya Kikamba:

**(2.8) Utambuzi wa Konsonanti za Kikamba.**

| **Fonimu** | **tahajia** | **jozi finyu** | **tafsiri** |
|---|---|---|---|
| /t/ | t | /ta:/ | taa |
| /k/ | k | /ka:/ | kijitu hiki |
| /ngj/ | ngy | /ngja/ | maskini |
| /č/ | ky | /ča/ | pambazuka |
| /ts/ | ts | /mbɛtsa/ | pesa |
| /ß/ | v | /mbɛva/ | jina la mtu |
| /ð/ | th | / ð ɛka/ | cheka |
| /nð/ | nth | /nð ɛkɛ/ | nyembamba |
| /s/ | s | / masɛɔ/ | mambo mazuri |
| /ɣ/ | gh | /maɣɛɔ/ | meno |
| /mb/ | mb | /vamba/ | sufi |
| /nd/ | nd | /vanda/ | panda |
| /nz/ | nz | /nzaana/ | kenge |
| /ŋg/ | ng | /ngaana/ | kilembwe |
| /m/ | m | /mata/ | mate |

| | | | |
|---|---|---|---|
| /n/ | n | /nata/ | maamkizi |
| /[ŋ/ | ny | /î ŋɔnga/ | nyonga |
| /ɲ/ | ng' | /î ɲɔɲa/ | mvuta mkia |
| /n/ | n | /kuna/ | piga |
| /l/ | l | / kula/ | kura |
| /w/ | w | /wanga/ | mpya |
| /j/ | y | /janga/ | mhogo |

Uwakilishi huu unadhihirisha kuwa, lugha ya Kikamba ina konsonanti ishirini na mbili (22). Tunatambua pia, konsonanti za Kikamba anghalabu hujitokeza mwanzoni mwa neno, au ndani na si mwisho wa neno. Utaratibu huu wa konsonanti, umebainishwa na uchanganuzi wa kimofolojia katika lugha za Kibantu.

Kutokana na sifa ya jinsi ya kutamka na pahali pa kutamkia, konsonanti za Kikamba huainishwa katika makundi saba na matano, mtawalia.. Zingatia jedwali lifuatalo la konsonanti. Ni vyema kutaja kuwa kilainisho cha kando /r/ hudhihirika katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili, kwa mfano: *kîlîvîtî* [keleßete] "kiberiti".

**(2.9) Jedwali la Konsonanti za Kikamba**

| Jinsi ya Kutamka | Mahali pa Kutamkia | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Midomoni | Menoni | Masineni | Burutioni | Kaakaani |
| vipasuo | | | t | | K |
| Vizuiwa | | | ts | ndʒ č | |
| vikwaruzo | β | ð | s | | ɣ |
| Nazali awali | mb | nð | nd nz | | Ŋg |
| Nazali | m | | n | ɲ | Ŋ |
| Kilainisho | | | l | | |
| viyeyusho | | | | J | W |

Sawa na vokali za Kikamba, konsonanti hudhihirisha maumbo tofauti. Maumbo hayo huwa sahili au changamano na pia huwakilishwa katika majedwali rusu.

Konsonanti sahili huwa na uhusiano wa moja kwa moja na rusu msingi. Kistari kimoja hutumika kuunganisha konsonanti na nafasi yake katika rusu msingi. Tazama konsonanti /w/ na /v/ katika maneno *wo* [wɔ] "kweli" na *va*? [βa] "wapi?

**(2.10) Kielelezo Jedwali cha Konsonanti Sahili**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu Msingi | K | K |
| | \| | \| |
| Rusu Fonimu | w | β |

Konsonanti changamano hutokea katika viwango viwili: utamkaji msingi na upili. Kiwango cha utamkaji msingi hurejelea nazali awali zinapojumuika. Mwambatano huu huwa na uhusiano wa mbili kwa moja na rusu msingi. Yaani vistari viwili hutumika kuunganisha umbo na rusu msingi. Zingatia konsonanti /ŋg/ na /nd/ katika maneno *ngũ* [ŋgo] "kuni" na *nda* [nda] "tumbo" ya yanadhihirisha umbo la konsonanti changamano msingi.

**(2.11) Kielelezo cha Konsonanti Changamano Msingi**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu Msingi | K | K |
| | /\ | /\ |
| Rusu Fonimu | ŋg | nd |

Umbo upili mara nyingi hutokea pale uyeyushaji wa vokali ya juu unatokea sanjari pa vokali nyingine. Matokeo ni mseto wa konsonsnti msingi na kiyeyusho. Konsonanti /mw/ na /mj/ katika maneno *mwaka* [mwaka] "mwaka" na *myaka* [mjaka] "miaka" zinadhihirisha umbo changamano upili.

**(2.12) Kielelezo cha Konsonanti Changamano Upili**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu Msingi | K | K |
| | / \ | / \ |
| Rusu Fonimu | mw | mj |

Umbo la nazalishi awali, uhusisha konsonanti ya umbo changamano la herufi tatu. Zingatia konsonanti /nzw/ na /ngj/ katika maneno kama *nzwa* [nzwa] "kumbikumbi" na *ngya* [ngja] "maskini" yanadhihirisha umbo hili.

**(2.13) Kielelezo cha Konsonanti ya Herufi Tatu**

| | | |
|---|---|---|
| Rusu msingi | K | K |
| | / \| \ | / \| \ |
| Rusu fonimu | nzw | ngj |

Uchanganuzi wa fonimu za Kikamba umetuelekeza kuwa vokali na konsonanti kwa jumla huchukua maumbo tofauti. Tumetambua pia kwamba, kila moja ya makundi haya ya fonimu yanabainishwa kimuundo. Uhusiano wa vokali na konsonanti utazidi kujitokeza katika uchanganuzi wa silabi.

### 2.1.4 Silabi za Kikamba


Silabi ni dhana ya kifonolojia inayorejelea ruwaza za fonimu katika maneno ya lugha kwa jumla (Taz Goldsmith 1990 na Crystal 1992). Wanaisimu wengi wanaelekea kukubaliana kwamba, muundo wa silabi una viungo vikuu viwili: tangulio (TA) na kina (KI). Kina nacho hugawanyika katika sehemu mbili yaani kilele (LE) na fungio (FU).



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Katika lugha ya Kikamba, vokali pekee ndiyo huchukua nafasi ya kilele. Kilele kwa hivyo ni kiungo pekee katika kina cha silabi. Lugha ya Kikamba kama zilivyo lugha zingine za Kibantu, hupendelea muundo wa silabi wazi. Tuzingatie muundo wa silabi katika neno *kana* "mtoto".

**(2.14) Vielelezo vya Muundo Silabi**




Silabi za Kikamba husawiri maumbo tofauti kutegemea mwambatano wa sauti. Kuna umbo la vokali (V) katika mwanzo wa maneno kama *ĩia* [eja] 'maziwa' ⟶ e & ja na *uma* [uma] "toka" ⟶ u & ma

**(2.15) Vielelezo vya Silabi ya Umbo la Vokali**



Kilele silabi chaweza kutanguliwa na konsonanti na kuleta umbo la konsonanti vokali (KV). Maneno ya silabi KV ni kama *ya* [ja] 'kula' na *ngo* [ŋgɔ] 'chui'.

**(2.16) Vielelezo vya Silabi la Umbo la KV**




Maumbo yaliyodhihirishwa hapo juu yanaonyesha fonolojia ya Kikamba hutumia silabi wazi, ilivyo katika lugha zingine za Kibantu.

Silabi wazi pia huweza kujidhihirisha katika jinsi mbili: nyepesi au nzito.

Silabi nyepesi inaundwa kwa kilele cha vokali sahili au changamano. Mifano katika lugha ya kikamba ni kama maneno *thi* [ð] "nenda" na *wo* [wɔ] "kweli

**(2.17) Kielelezo cha Silabi Nyepesi**

```
  SI                        SI
  /\                        /\
K   V                      K V
|   |                      | |
ð   i                      w ɔ
```

Silabi nzito huundwa kwa kilele cha vokali wakaa. Aina hii inadhihirika katika maneno ya Kikamba kama *saa* [sa:] "saa" na *too* [tɔ:] 'usingizi"

**(2.18) Kielelezo cha Silabi Nzito**

```
    SI                                        SI
    /\                                        /\
  K    vv                                   K    vv
  |    \/                                   |    \/
  s    a:                                   t    ɔ:
```

Baadhi ya maneno yenye maana kamili yamedhihirika kuundwa kwa silabi moja. Maneno mengine yanajmuisha silabi zaidi ya moja. Maneno mawili yenye silabi sawa yanaweza kubainishwa tu kupitia toni.

### 2.1.5 Toni Katika Maneno ya Kikamba.

Toni hueleza ruwaza za kidatu cha sauti katika kiwango cha neno (Taz Hambwe na Karanja 2004, na Odden 2005). Tutatumia dhana ya tonimu kuonyesha jinsi toni inavyosababisha utofauti wa kimaana katika leksimu za Kikamba. Tonimu ni ruwaza za toni zinazobainisha maana kileksika. Maneno ya Kikamba kama *Îia* [eia] "maziwa" / "gugu" na *veva* [ßɛßa] " roho" / "pumua" yanadhihirisha dhana ya tonimu.

**(2.19) Kielelezo cha Toni Bainifu**

a)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Rusu Msingi | V | KV | V | KV |
| Rusu Toni | C | J | J | C |

b)

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Rusu Msingi | V | KV | V | KV |
| Rusu Toni | C | J | J | C |

Tumetambua kuwa, kudhihirika kwa silabi wazi hujitokeza hata katika maneno mkopo ambayo awali yalijumuisha silabi funge. Maneno yafutayo ni mfano wa maneno mkopo yaliyozingatia muundo wa silabi wazi baada ya kutoholewa ili kudumisha muundo wa silabi katika lugha ya Kikamba.

**(2.20) Kielelezo cha Silabi Wazi**

| **Kiswahili** | | | **Kikamba** | |
|---|---|---|---|---|
| #alhamisi# | al $ ha $ mi $ si | ⟶ | #alamisi# | a $ la $ mi $ si |
| #labda# | lab $ da | ⟶ | #lavuta# | la $ vu $ ta |

Maelezo yetu pia yamebainisha kuwa, ubainifu wa kileksika unadhihirisha kwamba Kikamba ni lugha toni. Muundo wa kifonolojia katika lugha ya Kikamba unadhihirisha uhusiano wa vipashio na sifa za viwango tofauti. Vipengele vya kifonolojia vitadhihirisha uhusiano na muundo wa kimofolojia

## 2.2 Muundo wa Kimofolojia

Mofolojia ni taaluma ya kisarufi ambayo ina jukumu la kuyachunguza maumbo na mageuzi ya maneno (Taz Lyons 1968, 1981 na Mgullu 1999). Katika kuchunguza maneno, mofolojia hujihusisha na uundaji wa maneno ambapo huchunguza mofimu na alomofu ambazo huunda maneno. Tawi hili pia hujishughulisha na aina za maneno. Wanaisimu wengi wamekubaliana kuwa tawi hili laweza kugawanywa katika matawi mawili makuu; mofolojia ya minyambuliko ya maneno na mofolojia ya uundaji wa maneno. Kwa kuzingatia lengo la utafiti wetu, tutafafanua uainishaji wa nomino na uundaji wa nomino.

### 2.2.1 Nomino za Kikamba

Maneno ya lugha yoyote yanaweza kugawanywa katika aina majopo tofauti. Kila jopo pana lina vijopo. Kazi hii ililenga uainishaji wa nomino, uchanganuzi katika utafiti huu ulijikita katika nomino zilizokopwa kutokana na Kiswahili. Wasomi mbalimbali huainisha nomino kwa njia tatu ambazo ni taratibu za kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia (Taz Kioko 2005). Kazi hii, imeainisha ngeli za nomino kwa kutazingatia kigezo cha kimofolojia kinachojikita katika viambishi vya maneno. Miongoni mwa ngeli zilizopendekezwa na Welmers (1973) za Kibantu asili, ni kumi na saba (17) zilizowakilishwa katika lugha ya Kikamba.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

**(2.21) Ngeli za nomino**

| **Ngeli** | **Kiambishi ngeli** | **Mfano wa neno** | **Tafsiri** |
|---|---|---|---|
| 1 | /mo-/ | /mo-ndo/ | Mtu |
| 2 | /a-/ | /a-ndo/ | Watu |
| 3 | /mo-/ | /mo-te/ | Mti |
| 4 | /me-/ | /me-te/ | Miti |
| 5 | /e-/ | /e-to/ | Jani |
| 6 | /ma-/ | /ma-to/ | Majina |
| 7 | /ke-/ | /ke-vɛti/ | Mwanamke |
| 8 | /i-/ | /e -vɛti/ | Wanawake |
| 9 | /n-/ | / ɲ -omba/ | Nyumba |
| 10 | / n– / | / ɲ -omba/ | Nyumba |
| 11 | /o-/ | /o-lii/ | Uzi |
| 12 | /ka-/ | /ka-na/ | ~~Motto~~ mtoto |
| 13 | /to-/ | /to-ana/ | Watoto |
| 14 | /o-/ | /o-emi/ | Ukulima |
| 15 | /ko-/ | /ko-ema/ | Kulima |
| 16 | /ßa-/ | /ßa-ndo/ | Pahali |
| 17 | /ko-/ | /ko-ndo/ | Mahali |

Kutokana na mpangilio hapo juu, ni dhahiri kuwa nomino nyingi zinajitokeza katika vikundi vya umoja na wingi. Kwa mfano, ngeli ya pili ni wingi wa nomino zinazopatikana katika ngeli ya kwanza; ngeli ya nne ni wingi wa ngeli ya tatu; sita ni wingi wa tano; nane ni wingi wa saba; kumi ni wingi wa tisa; wingi wa ngeli ya kumi na moja unapatikana katika ngeli ya kumi na ngeli ya kumi na tatu wingi wake unajitokeza ngeli ya kumi na nne.

Japokuwa kuna ukariri wa viambishi ngeli, kwa mfano ngeli ya kwanza (1) na ngeli ya tatu (3), utofauti unaweza kuelezewa kisemantiki. Nomino katika ngeli ya 1 zinadhihirisha sifa za kibinadamu nayo majina katika ngeli ya 3 yanarejelea miti. Majina katika ngeli ya 9 na 10 ambayo yana kiambishi sawa, yanaweza kutofautishwa kwa kuzingatia ukubalifu wa kisarufi.

Mpangilio wa ngeli katika lugha ya Kikamba ni dhihirisho la nafasi ya uambishaji katika matumizi ya nomino. Umuhimu wa uambishaji utazidi kudhihirika katika uundaji wa nomino.

### 2.2.2 Uundaji wa Nomino

Mofolojia ya uundaji wa maneno ni mchakato unaotegemea kuweka viambishi katika mizizi ya maneno. Wakati viambishi mbalimbali vinapoongezwa katika mzizi wa neno, neno linalopatikana huwa jipya huundwa. Lugha nyingi za Kibantu huunda majina kutokana na aidha vitenzi, vivumishi au nomino zingine.

#### 2.2.2.1 Nomino Kutokana na Vitenzi

Uundaji wa majina katika lugha ya Kikamba hutokea zaidi kutokana na vitenzi. Uundaji huu husababisha majina yanayorejelea vitu kama michakato, dharura, hali na matokeo. Kimuundo, viambishi awili na viambishi tamati huongezewa mzizi wa kitenzi. Hebu tutazame mifano ifuatayo:-

**(2.22) Kielelezo Unominishaji wa Kitenzi**

| Kitenzi | nomino | Tafsiri |
|---|---|---|
| ĩma | mũ-ĩmi | Mkulima |
| | ũ-ĩmi | ukulima |
| soma | mũ -somi | msomi |
| | ũ -somi | usomi |
| nena | ũ–neni | unenaji |
| | mũ -neni | mnenaji |
| in | mw-ini | mwimbaji |
| | w-ini | uimbaji |

Data kutoka nyanjani ilidhihirisha kuwa zipo nomino za Kikamba ambazo zimeundwa kutokana na vitenzi vya Kiswahili. Nomino *Asomba* imeundwa kutokana na kitenzi cha Kiswahili "somba". Nomino *Asuini* imeundwa kutokana na kitenzi cha Kiswahili "zuia". Ufafanuzi wa dhana hii utajadiliwa zaidi katika sehemu ya uchanganuzi wa maneno mkopo.

#### 2.2.2.2 Nomino Kutokana na Vivumishi

Uundaji wa nomino kutokana na vivumishi katika lugha ya Kikamba uhusisha mfanyiko mmoja tu wa kuongezea viambishi awali. Mfanyiko huu uhusisha sana majina kutoka ngeli ya 14 ambayo hujumuisha majina ya udhahania.

**(2.23) Kielelezo cha Unominishaji wa Kivumishi**

| Kivumishi | Jina | Tafsiri |
|---|---|---|
| -nene | ũ-nene | ukubwa |
| -nini | ũ-nini | Udogo |
| -seo | ũ-seo | Uzuri |
| -theke | ũ-theke | Wembamba |
| -vya | ũ-vya | upya |

#### 2.2.2.3 Nomino Kutokana na Majina Mengine

Unominishaji wa nomino hutumia viambishi vya ngeli ya 5 na 6 kuundia majina dhalishi. Viambishi vya ngeli ya 12 na 13 navyo hutumika kuundia majina ya udogo. Mfano ufuatao unadhihirisha maana pana ya *mûndû* [mondo] "mtu"

**(2.24) Kielelezo cha Unominishaji wa Ukubwa na Udogo**

| Msingi Nomino | Nomino Tohozi | Tafsiri |
|---|---|---|
| | Ĩmũ-ndũ | Jitu |
| | Ma-mũ-ndũ | Majitu |
| mûndû | Ka-mũ-ndũ | Kijitu |
| | Tũ-mũ-ndũ | Vijitu |

Uchanganuzi wetu umedhihirisha unominishaji katika lugha ya Kikamba. Uundaji wa nomino za Kikamba kutokana na vitenzi unaonyesha uambishaji awali wa mzizi wa kitenzi. Nomino zilizoundwa zinaweza kuainishwa kimaana, kimuundo na pia kisintaksia. Tumetambua pia, kuwa baadhi ya nomino za Kikamba zimeundwa kutokana na maneno mkopo ya Kiswahili. Uundaji wa nomino kutokana na maneno mkopo ya Kiswahili, unafuata taratibu asili za uundaji wa nomino. Unominishaji husababisha uleksikali; nomino iundwayo ina maana ya kisemantiki. Nomino zote zinazoundwa katika misingi ya mofolojia ya Kikamba zaweza kuchanganuliwa kwa mtazamo wa muundo wa kisemantiki

**2.3 Muundo wa Kisemantiki**

Semantiki ni taaluma inayoshughulika na uchanganuzi wa maana. Dhana ya maana yaweza kutazamwa katika viwango tofauti kama vile semantiki leksia, semantiki tungo na kiwango cha muktadha. Kazi hii imeegemea zaidi semantiki leksia, kipashio muhimu

kikichukuliwa kama leksimu ( Taz Lyons 1977 na Cruse 1986, 2000). Leksimu katika kazi hii imechukua mtazamo wa orodha ya msamiati ubongoni mwa mzungumzaji asili wa lugha; kipashio kidogo ambacho kina uwezo wa kujisimamia peke yake kama kidahizo. Aidha maana lengwa katika kazi hii ni maana zile za kimsingi kulingana na nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo (SAM) (Taz 1.8). Leksimu zilizolengwa ni zile zinazofasiriwa kimaana na mzungumzaji asili wa lugha ya kikamba.

Uchanganuzi wa dhana ya maana huzingatia vipengele kama: fahiwa, urejeo na utambuzi katika kiwango cha leksimu na tungo. Ufafanuzi wetu umezingatia zaidi kipengele fahiwa huku kikichukuliwa kama dhana ya maana katika leksimu. Fahiwa katika leksimu au tungo yaweza kufafanuliwa katika misingi ya uhusiano kati ya wazo na dhamira kwa upande mmoja, na upande mwingine umuhimu wa usemi. Uchanganuzi wa fahiwa kiwango cha leksimu za luhga ya Kikamba umechukuliwa kama msingi wa muundo wa kisemantiki.

### 2.3.1 Muundo wa Leksimu

Kimsingi, maana ya leksimu yaweza kutazamwa katika mitazamo miwili: maana dhanishi na maana husishi. Matazamo uliochukuliwa katika kazi hii ni maana dhanishi. Wataalamu wa isimu wanaamini kuwa maana dhanishi ndiyo mtazamo mwafaka zaidi katika ufafanuzi wa muundo wa kisemantiki hasa kwa kuzingatia kuwa viwango vingine vya lugha kama fonolojia na sintaksia hudhihirisha muundo dhanishi wa alama za kiisimu

(Taz. Cruse 2000 Uk 126). Maana dhanishi ni jumla ya ufahamu unaowakilisha tamko la matukio na hali miongoni mwa mambo mengi.

Uchanganuzi wa leksimu za lugha ya Kikamba umechukua mtazamo kuwa maana dhanishi ni uhusiano kati ya dhana na alama za kiisimu. Kila leksimu ya lugha ya Kikamba, moja kwa moja uhusiana na dhana katika ulimwengu halisi. Uhusino wa leksimu na dhana katika lugha ya Kikamba waweza kuwa wa aina tatu: moja kwa moja, dhana nyingi kwa moja na leksimu nyingi kwa dhana moja.

Uhusiano wa moja kwa moja, hudhihirishwa na leksimu ambazo huwakilisha dhana moja; yaani uhusiano wa moja kwa moja kati ya leksimu na dhana. Mfano katika lugha ya Kikamba ni neno *singano* "sindano"

**(2.25) Kielelezo cha Uhusiano wa Moja kwa Moja**

*Singano* ⟶ kifaa chembamba, kirefu kiasi na chenye ncha

Kuna uhusiano wa dhana nyingi kwa leksimu moja. Uhusiano huu husababishwa na maneno yenye maana zaidi ya moja. Mfano katika lugha ya Kikamba ni neno *mbũi* "mbuzi"

**(2.26) Kielelzo cha Uhusiano wa Moja kwa Nyingi**


Kifaa cha kukunia nazi

*Mbũi*

mnyama

Umbo la tatu la kidhahania husababishwa na maneno tofauti ambayo huwakilisha dhana moja. Mfano katika lugha ya Kikamba ni neno *kũtũtia* "kutuacha", *kwîtwa* "kufa", *kũtwaa ndii mwakonî* "kupeleka nyuzi mjengoni" yote humaanisha *kũkwa* "kufa"

**(2.27) Kielelezo cha Nyingi kwa Moja**




Ufafanuzi wetu unatuwezesha kutambua kuwa muundo wa kisemantiki unasababishwa na uhusiano kati ya leksimu na dhana. Pia tunaweza kutambua kuwa uhusiano kati ya dhana ni kama kimia; leksimu moja huvuta dhana moja nayo dhana hiyo ikavuta dhana zingine nyingi. Tukio la jambo hili ni mahusiano ya kisemantiki ambayo twaweza kuyafananisha na wavu; yaani mahusiano ya fahiwa.

### 2.3.2 Mahusiano ya Fahiwa

Wataalamu wa isimu hutazama msamiati wa lugha kama mfumo wa leksimu ambazo zimefungamanishwa karibu na mahusiano ya fahiwa. Mahusiano haya ya kifahiwa huwa aina mbili; kiolezofaridi na usilisila (Taz Cruse 2000). Aidha kazi hii imefafanua uhusiano wa kiolezofaridi katika leksimu za Kikamba.

Muundo wa mfumo wa lugha ya Kikamba hutegemea kanuni ya uteuzi ambapo leksimu fulani huteuliwa kuandamana na leksimu nyingine katika sentensi. Uteuzi wa leksimu




KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

katika sentensi si wa kiholela bali hudhihirisha uhusiano wa kisemantiki. Aidha kiolezofaridi ni uteuzi wa leksimu unaozingatia mahusiano ya kisemantiki. Uhusiano huu wa kiolezofaridi katika leksimu za lugha ya Kikamba tumeutazama katika viwango vinne: hiponimia, meronemia, sinonimia na atonimia.

Hiponimia ni uhusiano wa ujumuisho; yaani uhusiano kati ya neno maalumu na neno la jumla. Hiponimia hudhihirisha uhusiano wa kihadhi wa fahiwa (Taz Lyons 1999 na Jackson na Amvela 2000). Maneno ya Kikamba kama *lĩu* "chakula", *isyo* "githeri", *makanda*, "githeri ambacho mahindi hayajatolewa maganda" *mũthokoî* "githeri ambacho mahindi yametolewa maganda", *mboka* "mboga", *nyama* "nyama" *maluu* "viazi" huonyesha uhusiano wa hiponimia.


**(2.28) Kielelezo cha Uhusiano wa Hiponimia**




Kielelezo hiki kinadhihirisha kuwa leksimu *lĩu* ni neno la jumla ambapo chini yake kuna maneno mengine kama *mũthokoî* yenye kulenga fahiwa zaidi. Tunatambua pia uhusiano wa hiponimia huonyesha leksimu kujitokeza katika viwango tofauti. Aidha uhusiano huu wa kihadhi ni wa taksonomi ambapo sifa bainifu ni viwango tofauti vya leksimu husika.


Mahusiano ya kisemantiki ambapo fahiwa moja ni sehemu ya fahiwa pana husababisha uhusiano wa meronimia. Mfano katika lugha ya Kikamba ni neno *mûtwe* ambalo hujumuisha sehemu tofauti kama *metho* "macho", *matû* "masikio", *manyûû* "pua", *mûnuka* "mdomo" na *matû* "mashavu"

**(2.29) Kielelezo cha Uhusiano wa Meronimia**




Uhusiano wa sinonimia hudhihirika wakati leksimu mbili zina fahiwa sawa (Taz Cann 1999, Kreider 20003 na Crystal 20005). Katika lugha ya Kikamba, baadhi ya leksimu hudhihirisha uhusiano huu: *kîandîki* na *kalamu* "kalamu"

**(2.30) Kielelezo cha Uhusiano wa Sinonimia**




Atonimia hubainisha uhusiano wa kinyume; yaani fahiwa fulani ni kinyume cha nyingine (Taz Palmer 1991 na Collinge 1990). Leksimu ambazo huwa na uhusiano wa atonimia

huwa kisemantiki haziwezi kujidhihirisha pamoja. Kielelezo kifuatacho chaonyesha mifano ya atonimia katika lugha ya Kikamba:

**(2.31) Kielelezo cha Uhusiano wa Atonimia**

| **Kikamba** | **tafsiri** |
|---|---|
| *ûngama* | simama |
| *îkala* | keti |
| *amûka* | amka |
| *koma* | lala |


Uchanganuzi wetu umebainisha kuwa leksimu za Kikamba hudhihirisha sifa za kisemantiki. Aidha sifa hizi za kisemantiki uhusiana na kusababisha kuhusiana kwa leksimu husika. Leksimu zinazohusiana zinaweza kuainishwa kwa kutegemea matazamo wa vikoa maana.

### 2.3.3 Vikoa Maana

Mahusiano ya kisemantiki husababisha leksimu kuunda wavu ambao umetawaliwa na mahusiano ya kifahiwa. Aidha mahusiano haya huunda vikoa maana; yaani maneno yaliyopangika katika makumbo ya maeneo au nyanja ambamo maneno hayo huwa yanahusiana sana kimaana (Taz Lyons 1977 na Loner 2002). Uchanganuzi wa awali umebainisha leksimu za Kikamba huingiliana kimaana na kuunda ruwaza za kimaana. Maingiliano haya ya karibu kimaana huunda vikoa maana tofauti huku vikoa hivyo

vikidhihirisha mawanda ya kisemantiki. Kwa mfano, majina ya jamii katika lugha ya Kikamba yataonyesha mahusiano kati ya leksimu tofauti :- *Mbaî* "jamii" *mũndũ* "mtu", *mũtumîa* "mme", *kîveti* "mke", *kavîsî* "kijana" *kelîtu* "msichana", *kana* "mtoto"

**(2.32) Kielelezo cha Kikoa Maana**




Katika lugha ya Kikamba, vikoa maaana vingine ambavyo hujumuisha maneno mkopo ni kama vifuatavyo:

**(2.33) Mifano ya Vikoa Maana**

| | **Kikamba** | **Kiswahili** |
|---|---|---|
| **Mimea** | *mũnathi* | mnazi |
| | *Mũtende* | mtende |
| | *mũembe* | mwembe |
| **chakula** | *mũsele* | mchele |
| | *sukalî* | sukari |
| | *ngũlu* | guru |

| | | |
|---|---|---|
| **wanyama** | *mbalasi* | farasi |
| | *mbaka* | paka |
| | *nyũmbũ* | nyumbu |

Uchanganuzi wetu watokana na baadhi ya leksimu zilizotoholewa kimaana kutokana na lugha ya Kiswahili. Tunaweza kusema kuwa maneno yaliyotoholewa kimaana yana uhusiano na maneno asili ya Kikamba kimaana; yaani yanaweza kuainishwa vikoa sawa na maneno asili.

Ufafanuzi wetu umedhihirisha kuwa leksimu za Kikamba ni ruwaza katika mfumo wa lugha yenyewe. Mfumo wa lugha daima hubadilika kutokana na leksimu ngeni kujipenyeza katika mfumo huo aidha kupitia ukopaji au neno kuchakaa (Taz 1.7). Leksimu ngeni inapojipenyeza katika mfumo wa lugha, aidha huchukua nafasi ya leksimu awali au ikasababisha kufinyika kwa fahiwa ya leksimu awali. Leksimu katika kikoa maana fulani pia yaweza kupanuka kimaana na hivyo kusababisha kufinyika kwa fahiwa ya leksimu jirani. Mifanyiko hii yote ya kifahiwa husababisha swala la ualama.

### 2.3.4 Ualama

Dhana ya ualama tumeifafanua kwa kuegemea muundo wa leksika. Katika mtazamo huu, ualama waweza kutazamwa viwango vitatu: ualama mofolojia, ualama msambao na ualama maana. Utafiti wetu umefafanua viwango viwili vya mwisho. Lugha ya Kikamba hudhihirisha ualama msambao ambapo leksimu yenye ualama hujitokeza katika muktadha finyu. Kwa mfano, leksimu *matuku* na *taliki* yote ni maneno ambayo hutumika kuleta maana ya tarehe kwa jumla. Neno *taliki* ni la mkopo (tarehe); kulingana na

matumizi yake, neno hili lilikopwa kutekeleza maana msingi. Tufafanue zaidi kwa kutumia sentensi zifuatazo:-

**(2.34)**

| | | |
|---|---|---|
| i. | *Twî matũkũ meana ata?* | "tuko tarehe ngapi?" |
| ii. | *Matũkũ aa syîndũ syîna vinya* | "siku hizi vitu ni ghali" |
| iii. | *Matũkũ maku nî matale* | "siku zako zimehesabiwa" |

Katika sentesensi ya kwanza, neno *matũkũ* laleta maana ya tarehe; sentensi ya pili, dhana ya hali ya maisha kuwa magumu na sentensi ya tatu, dhana ya onyo hasa kwa mtenda maovu.

**(2.35)**

| | | |
|---|---|---|
| i. | *Ngoka taliki itatu mwai wa mbee* | "nitakuja tarehe tatu mwezi wa kwanza" |
| ii. | *Twî taliki siana ata?* | "ni tarehe ngapi?" |

Sentensi zote mbili zaleta maana sawa ya neno *taliki* – terehe. Kati ya leksimu hizi mbili *matuku* na *taliki*, neno *matuku* halina ualama msambao ilhali ualama msambao wadhihirika katika leksimu *taliki.*

Leksimu za Kikamba pia zaweza kuchukua ualama maana. Ualama maana hutokea wakati leksimu moja inalenga zaidi fahiwa kuliko leksimu kinyume. Mfano wa Kikamba ni neno *moi* (ng'ombe jike) na *ng'ombe* (ng'ombe). Neno *moi* yalenga zaidi fahiwa na hivyo kuwa na ualama maana. Mifano mingine ya kikamba ni kama ifuatayo :-



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

| **Hayana ualama maana** | **Ualama maana** |
|---|---|
| *ĩlũnga* | *ndũũme* (kondoo dume) |
| *mbũi* | *mbaika* (mbuzi jike) |
| *ngũkũ* | *nzamba* (kuku dume) |

Uchanganuzi wetu umedhihirisha kuwa leksimu za Kikamba hudhihirisha ualama msambao na ualama maana. Tunaweza kudai kuwa kigezo cha aidha leksimu kujitokeza kuwa na ualama maana au ualama msambao huwa muhimu kwa mzungumzaji wa Kikamba katika kufanikisha maana iliyokusudiwa katika mawasiliano.

### 2.3.5 Dhana ya Muktadha

Pendekezo la baadhi ya wanaisimu ni uzingativu wa muktadha wa lugha katika kutalii maana ya leksimu. Aidha, maneno katika hali yao ya upekee hayapashi ujumbe kikamilifu japokuwa yana fahiwa; maneno hayatumiki katika ombwe tupu sharti yaandamane na vipashio vingine vya kisemantiki ili ujumbe ukamilike (Taz Cruse 2000). Leksimu huwa na uwezo wa kudhihirisha maana tofauti kutegemea muktadha. Wazo hili laweza kudhihirishwa kwa kutazama maneno ya Kikamba: *mwaitũ* "mama" na *kĩndũ* "kitu" katika jozi la sentensi zifuatazo:

i. *Mwaitũ nũkũeya ngewa na syana syake* "mama anazungumza na wanawe"

ii. *Kilya mwaitũ nĩngũũthowea maiyũ* "nyamaza *mwaitũ* nitakununulia ndizi"

Neno *Mwaitũ* katika sentensi ya kwanza, laleta maana ya mzazi wa kike ilhali katika sentensi ya pili neno hilo laleta maana ya mtoto wa kike.

i. *Kîndũ waku nũvikie?* "mtu wako amefika?"

ii. *Nînakuetea kila Kîndũ kyaku* "nimekuletea kile kitu chako"

Neno *Kîndũ* katika sentensi ya kwanza, laleta maana ya mpenzi ilhali katika sentensi ya pili neno hilo laleta maana ya kitu fulani kinachofahamika na wale wanaowasiliana.

Ufafanuzi wetu unatuelekeza kutambua kuwa jamii ya Wakamba hutegemea kigezo cha muktadha kutofautisha maana ya leksimu katika mawasiliano. Ujumbe wa maneno yenye uhusiano wa polisimia kwa mfano, utabainishwa kupitia muktadha.

**Hitimisho**

Uchanganuzi wa vokali katika lugha ya Kikamba kwa mtazamo wa fonolojia vipandesauti huru, umedhihirisha kuwa maumbo tofauti ya vokali hutegemea muda wa kuitamka vokali hiyo. Vokali za Kikamba hudhihirisha maana tofauti katika leksia kutegemea wakaa. Sifa hizi za kifonolojia zinajitokeza pia katika konsonanti za Kikamba. Kulingana na ufafanuzi wetu, maneno mkopo yametoholewa ili yadumishe muundo wa kifonolojia wa lugha kopaji. Aidha, maneno mkopo yamejumuishwa katika ngeli asili za Kikamba na wala hayajaunda ngeli geni. Muundo wa silabi wazi unajumuisha hata maneno mkopo ambayo aidha awali hayakudhihirisha muundo wazi. Katika uundaji wa maneno, tumeonyesha kuwa majina yaliyoundwa kutokana na vitenzi vya Kiswahili yamefuata utaratibu wa uundaji wa majina katika lugha ya Kikamba. Tumeonyesha kuwa kipengele cha toni ni muhimu katika kutofautisha maana katika maneno yenye umbo

# SURA YA TATU

# MISINGI YA UTOHOZI MAANA

## Kitangulizi

Sura iliyotangulia ilishughulikia muundo wa maneno ya Kikamba, kwa kuegemea sifa za kisarufi katika tanzu za fonolojia, mofolojia na semantiki.Uchanganuzi katika sura hii umetazama utohozi semantiki kama mchakato unaotawaliwa na kanuni na taratibu. Lugha zote ulimwenguni zimeundwa kwa maana mbili za kimsingi: maana dhanishi na maana tagusani (Taz 1.8.2). Utafiti huu ulizingatia mtazamo huo katika juhudi za ufafanuzi wa kanuni zilizopelekea maneno mkopo ya Kikamba kuchukua mikondo tofauti ya kimaana. Mtazamo wa kanuni kuelekeza taratibu katika mchakato husika ulipelekea uchanganuzi katika sura hii kuwekwa katika sehemu mbili: kanuni za utohozi maana, na taratibu za utohozi maana.

## 3.1 Kanuni za Utohozi Maana

Swala la kanuni za utohozi maana limejadiliwa na baadhi ya wanaisimu ambao wanashikilia kuwa, zipo kanuni bia ambazo huelekeza mikondo ya maana; yaani hali ya kubanika au kupanuka kwa fahiwa ya leksimu fulani (Taz Anttila 1972 na Mc Mahon 1996). Tunaweza kudai kuwa, kanuni bia ni sheria zinazoaminika kusababisha aidha upanukaji au ufinyizi wa maana.

Nadharia ya Tahakiki Usemi na Sarufi Amilishi Mfumo zakubaliana kuwa, nanga ya maana za kimsingi katika mawasiliano hujikita katika hali ya lugha kusimba tajiriba za kitamaduni na kijamii na ufasili wa maana kutegemea vikwazo vya kijamii. Aidha vikwazo vya kijamii baadhi huwa ni vya kiisimu na baadhi si vya kiisimu (Taz 1.8.1 na 1.8.2). Mtazamo huu ulitueleza kubaini kuwa aidha kupanuka kwa fahiwa kunaweza kusababishwa na mfumo wa kawaida wa lugha; ukuaji wa lugha. Tulitambua pia ukopaji wa leksimu ni sababu nyingine ya kupanuka au kufinyika kwa fahiwa za leksimu; wanajamii wa lugha kopaji hufasiri maana za maneno mkopo huku vikwazo vya kijamii vikielekeza kufasiri huko. Uchanganuzi wetu ulilenga mfanyiko wa ukopaji wa kisemantiki ambao ulionekana kusababisha kupanuka na kufinyika kwa fahiwa za maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Utafiti wetu ulidhihirisha kanuni za utohozi maana zifuatazo:

1. Kanuni za kiisimu
2. Kanuni za kijamii
3. Kanuni za kihistoria

### 3.1.1 Kanuni za Kiisimu

Kanuni za kiisimu huegemea vigezo vya kiisimu ambavyo husababishwa na mfumo wa lugha. Tulidokeza awali kuwa uzalishaji matini kwa upande mmoja hutegemea vikwazo vya kiisimu; yaani mfumo wa lugha (Taz 1.8.1). Kimsingi, kazi hii imejadili vigezo viwili: mchakato wa unominishaji na hali ya lugha. Unominishaji ni mchakato ambao hutokea katika mfumo wa lugha kwa lengo la kunominisha vifaa vipya aidha kutokana na

teknolojia geni au leksimu za zamani zinapohisika kuchakaa na wanajamii. Leksimu uhisika kuchakaa wakati fahiwa yake inapokosa ule uzito wa kuwasilisha ujumbe unaotarajiwa na wanajamii (Taz Lyons 1977). Maadamu tumejadili unominishaji hudhihirika katika lugha ya Kikamba (Taz 2.2). Uchanganuzi wetu umeangazia unominishaji kupitia ukopaji.

Mtagusano wa Kikamba na Kiswahili umesababisha kusambaa kwa vifaa kutoka utamaduni wa Kiswahili hadi utamaduni wa Kikamba. Aidha lugha ya Kikamba imebidika kuvinominisha vifaa vipya kutokana na ukopaji. Baadhi ya unominishaji huu umefuata mkondo wa ukopaji wa leksimu. Mfanyiko wa ukopaji kwa lengo la unominishaji uhusisha maana msingi huku maana ziada ikipuuziliwa mbali Anttila (Ibid). Ukopaji wa maana msingi huku maana ziada ikiachwa, husababisha ufinyizi wa maana. zifuatazo ni mifano ya bidhaa zilizosambaa kutoka Uswahilini hadi Ukambani:

| **(3.1)** | **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|---|
| | nyanya | > | înyanya |
| | korosho | > | koloso |
| | baba | > | vava |
| | Wallah! | > | walaî |

Leksimu *înyanya* katika lugha ya Kikamba ni mfano wa maneno mkopo yaliyofuata utaratibu wa ufinyizi. Neno *înyanya* katika lugha ya Kikamba hurejelea tunda la mnyanya. Leksimu *înyanya* latokana na neno la Kiswahili “nyanya” ambalo hurejelea

tunda la mnyanya na pia mama mzaa baba au mama; bibi. Ukopaji wa neno *înyanya* uliandamana na ukopaji wa mmea mnyanya ambao awali haukupatikana mazingirani mwa lugha ya Kikamba.

Mfanyiko wa kimofolojia pia uliandamana na utohozi maana wa leksimu *înyanya.* Katika hali ya umoja, kiambishi *î* kimeongezewa ili kuafiki muundo wa kimofolojia wa lugha ya Kikamba. Katika hali ya wingi, kiambishi *m* yaani *manyanya* kimeongezewa. Licha ya utohozi maana, neno *înyanya* limetoholewa kimofolojia.

Neno *koloso* ni mfano mwingine wa ufinyizi maana. Leksimu *koloso* katika lugha ya Kikamba hurejelea mbegu ya bibo itokanayo na mti wa mkanju. Neno *koloso* latokana na neno la Kiswahili "korosho". Neno "korosho" katika lugha ya Kiswahili hurejelea mbegu ya bibo itokanayo na mti wa mkanju na pia hurejelea pambo lililotokeza kwenye usukani wa mtepe. Ukopaji wa leksimu "korosho" umesababisha ufinyizi maana ambapo maana msingi ndiyo iliyokopwa.

Utohozi wa kifonolojia unadhihirika katika ukopaji wa leksimu "korosho". Fonimu [*r*] imetoholewa na kuwa fonimu [*l*] kwa sababu fonimu [*r*] si mojawapo ya konsonanti za Kikamba ila hujitokeza nadra katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Ni rahisi nafasi ya fonimu [*r*] kuchukuliwa na fonimu [*l*] kwa sababu sauti zote ni vilainisho. Fonimu [*h*] imedondoshwa. Neno korosho limetoholewa kimaana na pia kifonolojia ili kuafiki muundo wa kifonolojia wa lugha ya Kikamba.

Kutokana na maelezo yetu, tunaweza kudai kuwa mchakato wa unominishaji ambao ni kigezo cha kiisimu, umechangia baadhi ya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili kuchukua utaratibu wa ufinyizi maana; yaani kusambaa kwa vitu kutoka Uswahilini hadi Ukambani kumesababisha lugha ya Kikamba kuvinominisha vitu hivyo kupitia ukopaji wa leksimu.

Kigezo cha hali ya lugha tumekichanganua kwa kuzingatia vipengele viwili: hali ya maneno kuwa polisemiki na unasibu wa alama za kiisimu. Maneno kuwa polisemiki ni kuwa na uwezo wa kupanuka au kubanika kwa fahiwa. Neno linapopoteza umaarufu wake miongoni mwa wanajamii, maana ya neno hilo hufinyika na wakati mwingine likadondoshwa katika miktadha ya lugha. Aidha, umaarufu wa neno uzidipo, maana yake hupanuka huku neno lile likitumika katika miktadha mipana (Taz Mc Mahon 1994). Kutegemea sababu ya ukopaji, umaarufu wa neno mkopo waweza kuzidi au kupungua. Kutokana na hali ya polisemiki, umaarufu wa neno mkopo uzidipo kutakuwa na uwezekano wa neno hilo kutumika katika miktadha mipana.

Leksimu *vava* ni mfano wa maneno mkopo ambayo umaarufu wake umezidi miongoni mwa jamii iliyohojiwa. Leksimu *vava* katika lugha ya Kikamba hurejelea mzazi wa kiume na pia hutumika kama jina la heshima la kumrejelea shemeji upande wa mumeo; yaani jina badala. Ni mwiko miongoni mwa jamii iliyohojiwa kuwataja ndugu za mumeo kwa jina lao hasa walio wakubwa kuliko mumeo. Neno asili lililotumika kuwatajia

mashemeji nduguze mumeo lilikuwa *Ûkûlû.* Leksimu *vava* yatokana na neno la Kiswahili "baba". Katika lugha ya Kiswahili, neno "baba" hurejelea mzazi wa kiume pia hutumika kama jina la heshima kumaanisha laweza kurejelea mtu yeyote apewaye heshima tofauti na lugha ya Kikamba ambapo hutoa heshima kwa mtu maalumu. Kutokana na hali ya polisemiki ya neno *vava*, limepanuka kimaana.

Baadhi ya wanaisimu hushikilia mtazamo kuwa uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa ni wa kinasibu; yaani kiashiria chochote chaweza kutumika kuashiria kitu chochote katika ulimwengu halisi. Kwa kuzingatia mtazamo huu, uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa waweza kubadilika wakati wowote (Taz Mc Mahon Ibid na Mgullu 2004). Kigezo hiki cha kiisimu kimesababisha jamii kopaji ya Wakamba kubadili baadhi ya maana ya leksimu zilizokopwa.

Neno *walaî* ni mfano wa leksimu mkopo ambalo maana imebadilishwa. Katika lugha ya Kikamba, leksimu *walaî* hurejelea aina ya kofia ambayo huaminika kuvaliwa na watu wenye imani ya Kiislamu. Leksimu *walaî* latokana na neno la Kiswahili wallah!. Neno wallah! katika lugha ya Kiswahili hurejelea tamko ambalo mtu hutamka kusisitiza asemalo ni kweli. Maana ya tamko wallah! imesogea kumaanisha kofia kwa sababu uhusiano kati ya kiashiria na kiashiriwa ni wa kinasibu. Hali ya unasibu wa alama za kiisimu kwa jumla ni kipengele ambacho kimechangia uwezekano wa baadhi ya maneno mkopo ya Kikamba kuchukua mkondo wa usogezi maana baada ya kutoholewa kimaana.

Uchanganuzi huu ulituelekeza kubaini kuwa lugha ya Kikamba imetumia tajiriba za kitamaduni na kijamii kuelekeza aidha maana ya maneno mkopo au kuvinominisha vifaa vilivyokopwa kutokana na lugha ya Kiswahili. Tunaweza kusema kuwa, mfumo wa lugha ya Kikamba umewezesha baadhi ya maneno mkopo ya Kikamba kuchukua mikondo tofauti ya maana ikilinganishwa na awali.

### 3.1.2 Kanuni za Kijamii

Kanuni za kijamii ni jumla ya vikwazo vya kijamii ambavyo huathiri uzalishaji wa matini (Taz 1.8.1). wanajamii waliohojiwa walionekana kudumisha kaida za kijamii katika matumizi ya lugha ili kudumisha mahusiano ya kijamii. Katika juhudi za kuzalisha na kutafsiri matini, maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yalionekana kuzalishwa na wanajamii huku maana ikipanuliwa au kubanika kutegemea kaida za jamii. Kimsingi, tulibainisha maswala matatu ya kijamii: nia ya jamii, desturi na dini. Maswala haya yalibainishwa na data ifuatayo.

| (3.2) | **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|---|
| | Kimba | > | kimba |
| | Maiti | > | maiti |
| | Buku | > | îvuku |
| | Ishmael | > | Sumaili |

Nia ya jamii kwa kuegemea mkabala wa lugha ni mshawasha wa kindani unaosababishwa na kichocheo cha aina fulani ambacho hukifanya kiumbe kusema au

kutenda jambo fulani (Taz Fasold 1984). Aidha nia ya wanajamii kuhusu leksimu fulani husababisha maana ya leksimu hiyo kubadilika kutegemea jinsi wanajamii hao wanavyothamini matumizi ya leksimu hiyo katika mawasiliano (Taz Mc Mahon 1994 uk 179). Mfano katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili ni; *kimba* 'kimba' na *maiti* 'maiti'.

Leksimu *kimba* na *maiti* katika lugha ya Kikamba yametoholewa kurejelea vitu tofauti japokuwa katika lugha ya Kiswahili leksimu hizi hurejelea mtu mfu kwa jumla. Ni vyema tutaje kuwa, katika lugha ya Kiswahili leksimu "kimba" lina maana zaidi; hutumika kurejelea fungu au shonde la kinyesi cha mtu au myama na pia hurejelea gimba yaani umbo la kitu au mtu lionyeshalo mjengo au unene wake.

Neno *kimba* katika lugha ya Kikamba hurejelea mzoga yaani mwili wa mnyama aliyekufa. Leksimu *maiti* katika lugha ya Kikamba ndiyo hutumika kurejelea mtu mfu. Neno asili ambalo hutumika pamoja na neno mkopo kurejelea mtu mfu ni *mwĩĩ* huku neno mkopo *maiti* likichukua nafasi ya ualama msambao. Nia ya wanajamii wa eneo la utafiti limesababisha usogezi maana wa neno *kimba.* Yaani nuia ya kuleta dhana tofauti katika kutofautisha urejeleaji wa binaadamu mfu na mnyama ambaye hana uhai.

Uchanganuzi wetu umedhihirisha kuwa nia ya wanajamii kuhusu leksimu fulani yaweza kusababisha udhalilishajimaana au uemeshajimaana. Mfano tuliojadili yaani leksimu *kimba* unaegemea udhalilishajimaana.

Mila na desturi za jamii fulani huelekeza mfumo wa maisha wa jamii husika. Kwa mfano, kutaja jina la wakwe au mashemeji ni mwiko miongoni mwa jamii nyingi (Taz Crowly 1997). Tumedokeza ni mwiko miongoni mwa jamii ya Wakamba kuwataja wakwe au mashemeji upande wa mumeo kwa jina. Aidha mtu aolewapo, hulazimika kuibuka na majina badala ya kurejelea nduguze mume wake. Utafiti ulibainisha kuwa majina mbadala kwa kawaida yalizuliwa kwa kuzingatia sifa bainifu za mtu apewaye jina; aidha sifa za kimaumbile au tabia. Kwa mfano, jina *mûasa* "mrefu" lilipewa mtu mwenye sifa za urefu. Kutokana na jaribio hili la kimila na desturi jamii katika eneo la utafiti lilikopa nomino yoyote ya Kiswahili kutekeleza desturi hii ya Wakamba. Utafiti nyanjani ulidhihirisha matumizi ya nomino kutokana na lugha ya Kiswahili katika kurejelea mtu hata kama nomino hizo katika lugha ya Kiswahili hazikutumika kurejelea mtu. Mfano wa neno la Kikamba kutoka Kiswahili ambalo hutumika kumrejelea mtu ni *kavuku*.

Leksimu *kavuku* yatokana na neno la Kiswahili "buku". Neno "buku" katika lugha ya Kiswahili hurejelea panya mkubwa mwenye mkia kama ndezi na pia hurejelea kitabu kilichopigwa chapa kwa herufi za Kirumi. Neno *kavuku* katika lugha ya Kikamba hurejelea mtu kama jina la pekee. Mmoja wa wahojiwa alisema kuwa watu wa ukoo wao walitumia leksimu *kavuku* kama jina badala la kumrejelea ndugu mkubwa wa mume wake. Kwa kawaida mwanamke wa kwanza kuolewa katika boma, majina aliyowapa nduguze mume wake ndiyo yaliyotumiwa na watu wa ukoo. Wakati mwingine majina mbadala yalikita mizizi kutegemea umaarufu wa mtu mwenye jina hilo na kuwa majina rasmi ya ukoo.

Leksimu *îvuku* katika lugha ya Kikamba pia yatokana na neno "buku". Neno *îvuku* katika lugha ya Kikamba hurejelea kitabu aidha kilichochapishwa au daftari; yaani kitabu cha kuandikia. Matumizi ya leksimu *îvuku* katika lugha ya Kikamba yanadhihirisha kupanuka kwa fahiwa kwa sababu hurejelea jumla ya vitabu vyote.

Ufafanuzi wa leksimu *kavuku* na *îvuku* unatuelekeza kutambua kuwa kigezo cha mwiko ambacho ni cha kijamii kimechangia baadhi ya taratibu za utohozi maana ya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Matumizi ya leksimu *kavuku* yanadhihirisha usogezi maana. Maneno *kavuku* na *îvuku* pia yametoholewa kifonolojia; fonimu [b] imetoholewa na kuwa fonimu [ß] ambapo zote ni fonimu za menoni. Utohozi wa kimofolojia pia unadhihirika. Kiambishi *ka* cha udunishaji katika lugha ya Kikamba kimeongezwa katika neno *kavuku* na kiambishi *î* cha ukubwa kimeongezwa katika neno *îvuku*.

Dini ya Kiislamu ni kipengele kingine ambacho kimesababisha kuenea kwa lugha ya Kiswahili katika eneo la utafiti (Taz Mbaabu1995). Utafiti nyanjani ulidhihirisha kuwa baadhi ya jamii katika eneo la utafiti hasa mji wa Kitui na viunga vyake imesilimishwa. Kusilimishwa huandamana na kupewa jina jipya la Kiislimu. Waliosilimishwa huienzi lugha ya Kiswahili na hivyo kuchangia matumizi yake katika mawasiliano. Kutokana na hali hii, majina ya Kiislamu kuwarejelea waliosilimishwa yamesambaa. Hali ya kuitukuza lugha ya Kiswahili imesababisha majina ya Kiislamu ambayo hurejelea mtu

kutumika pia kurejelea mahali. Mfano wa jina la Kikamba ni *Sumaili* kutokana na jina la Kiswahili "Ishmael".

Leksimu *Sumaili* katika lugha ya Kikamba hutumika kurejelea mtu ambaye imani yake ni ya Kiislamu na pia hutumika kurejelea mahali. Matumizi ya leksimu hii yamepanuka na pia kusogea. Kwa jumla, kusambaa kwa dini ya Kiislamu kumeandamana na ufahari wa lugha ya Kiswahili miongoni mwa jamii iliyohojiwa. Matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili kwa upande mwingine kumechangia kupanuka maana kwa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili.

Uchanganuzi wetu ulituelekeza kutambua kuwa kupanuka au kufinyika kwa maana ya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili ni zao la wanajamii wa Kikamba. Maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili yamefasiliwa na jamii ya Wakamba kutegemea mtazamo wa maisha, imani na mielekeo ya wanajamii.

### 3.1.3 Kanuni za Kihistoria

Rekodi za kihistoria kama tulivyodokeza zadhihirisha mtagusano wa kipindi kirefu kati ya lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili (Taz Ogot 1976 na Spear 1981). Biashara ya Watumwa na pembe za ndovu ni mojawapo ya matukio ya kihistoria ambayo yalisababisha mtagusano kati ya lugha hizi mbili. Tukio hili la kihistoria lilisababisha mtagusano wa kitamaduni na hivyo vifaa vingi kutoka pwani vikasambaa eneo la Ukambani.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

| (3.4) | **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|---|
| | chumvi | > | mûnyû |
| | shanga | > | wanyoa |
| | kamba | > | îkanda |
| | kisu | > | ûvyû |

Jumla ya vifaa kutoka pwani ni pamoja na mapambo, mavazi na vifaa vya kiteknolojia. Kusambaa kwa vifaa hivi Ukambani kuliandamana na ukopaji wa leksimu ili kuvirejelea vifaa vyenyewe. Ukopaji wa leksimu kurejelea vifaa vilivyokopwa umechukua mikondo tofauti ya utohozi maana kutegemea kifaa husika na sababu za ukopaji. Mfano wa bidhaa kutoka pwani hadi ukambani ni "chumvi". Neno "chumvi" halikukopwa pamoja na kusambaa kwa kiungo "chumvi" ila neno asili *mûnyû* lilitumika kurejelea kiungo "chumvi".

Leksimu *mûnyû* katika lugha ya Kikamba ilitumika kurejelea aina ya masalio ya mchanga baada ya kuchunjwa kwa maji ambayo yalitumika kama "chumvi". Aina hii ya mchanga huitwa *kîthaayo*. Kwa sasa mifugo ndio hutumia mchanga huo. Tunaweza kusema kuwa utaratibu huu ni wa aina ya urari wa umbo, ambapo umbo asili la neno linatumika kurejelea maana geni kutokana na kusambaa kwa kifaa katika lugha kopaji.

Leksimu *wanyoa* ni mfano mwingine uliochukua utaratibu wa urari. Katika lugha ya Kikamba, neno *wanyoa* lilitumika kurejelea pambo "ushanga" ambalo lilitengenezwa

kwa shanga ndogo za miti. Neno *ngalîa* katika lugha ya Kikamba lilitumika kurejelea ushaga uliotengenezwa kwa shanga kubwa za miti. Pambo "ushanga" liliposambaa kutoka pwani, leksimu "ushanga" haikukopwa ila maneno asili yalitumika kurejelea pambo hili kwa sababu ni pambo ambalo awali lilipatikana katika utamaduni wa lugha ya Kikamba. Kutokana na kusambaa kwa aina moja ya pambo kutoka pwani yaani "ushanga", kukazuka aina tatu za mapambo miongoni mwa jamii kopaji; *wanyoa* ushanga mdogo, *ngalîa* ushanga wastani na *masole* ushanga mkubwa. Aidha lugha ya Kiswahili hutumia leksimu "ushanga" kurejelea mapambo yote yaliyotengenezwa kwa shanga hata kama ni ndogo.

Uchanganuzi wetu unatuelekeza kudai kuwa mtagusano wa kitamaduni kutokana na matukio ya kihistoria husababisha utohozi maana kutegemea ulinganifu au utofauti wa kitamaduni. Ulinganifu wa kitamaduni kati ya lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili umesababisha utohozi maana kuchukua mkondo wa urari wa umbo. Utofauti wa kitamaduni kwa upande mwingine umesababisha utohozi maana wa maneno mkopo ya Kiamba kutoka Kiswahili kuchukua mkondo aidha wa ufinyizi au upanukaji maana.

Ufafanuzi wa data ulibainisha kuwa kanuni bia za kiisimu, kijamii na kihistoria zimesababisha kuzalishwa upya kwa maana za maneno mkopo. Aidha maana ya maneno mkopo imebanika, kupanuka au kusogea. Tumetambua pia kanuni bia hizi hushirikiana katika kubadili maana za maneno. Maelezo kuhusu leksimu *walaî* yanaweza kujadiliwa kusababishwa na vikwazo vya kijamii au vikwazo vya kiiisimu. Aidha ni vigumu

kuwekea kanuni bia mipaka katika mchakato wa taratibu za utohozi maana. aidha mtazamo huu unaafiki mtazamo wa nadharia ya Tahakiki Usemi kuwa mfumo wa lugha ni sehemu ya mfumo wa jamii. Uchanganuzi ufuatao wa taratibu za utohozi maana ulibainisha kuwa kanuni bia hushirikiana katika kufanikisha mabadiliko ya maana za maneno.

### 3.2 Taratibu za Utohozi Maana

Taratibu za utohozi maana ni mbinu, njia au mifanyiko ya kisemantiki inayotumiwa kutohoa maana za maneno. Baadhi ya wanaisimu wameujadili utohozi wa leksimu kama mfanyiko wa kisemantiki ambapo leksimu mkopo hukopwa kwa lengo la kujaliza maana ambayo haipatikani katika lugha kopaji. Kanuni tulizofafanua husababisha fahiwa ya leksimu mkopo kubadilika pasipo kubadili umbo la leksimu hiyo (Taz 3.1). Utohozi wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili unaweza kudhihirika katika mbinu zifuatazo:

1. Ufinyizi maana
2. Usogezi maana
3. Upanuzi maaana
4. Urari wa umbo

#### 3.2.1 Ufinyizi Maana

Mbinu ya ufinyizi maana husababisha kubanika kwa fahiwa. Aidha maana msingi ya leksimu mkopo hutolewa huku maana ziada zikiachwa (Taz Anttila 1972). Kutegemea

data iliyopatikana nyanjani, mbinu hii yaweza kuchanganuliwa kwa kugawa vitengo vifuatavyo.

1. Nomino za vifaa
2. Nomino za mavazi
3. Nomino za mahali
4. Nomino za zingine

#### 3.2.1.1 Vifaa

Kifaa ni neno litumiwalo kurejelea kitu au chombo kinachotumika katika kufanyia kazi fulani au kutekeleza kusudi fulani.

**(3.4)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| kekee | > | *kekee* |
| randa | > | *landa* |
| kikombe | > | *kĩkombe* |
| chupa | > | *suva* |

Neno *kekee* hutumiwa katika lugha ya Kikamba kurejelea kifaa cha seremala. Matumizi yake katika lugha ya Kiswahili hurejelea kifaa cha seremala na pambo la kike livaliwalo kama kikuku au bangili. Maana iliyotoholewa ni maana msingi tu huku maana ziada ikiachwa.

*Landa* ni leksimu inayotumiwa kurejelea kifaa cha seremala katika lugha ya Kikamba. Maana ya leksimu hii katika lugha ya Kiswahili hurejelea kifaa cha seremala na kitendo cha kufanya kifaa kuwa sawa. Sawa na leksimu *kekee*, maana msingi ndiyo iliyotoholewa hivyo kusababisha ufinyizi maana wa leksimu *Landa*.

Neno *kîkombe* katika lugha ya Kikamba hurejelea chombo cha kunywea na pia hutumika kurejelea sehemu ya katikati ya gurudumu la baiskeli inayoshika gololi. Katika lugha changizi ya Kiswahili, leksimu "kikombe" hurejelea dhana nne tofauti; hurejelea chombo kitumiwacho kunywea, chombo maalumu kishindaniwacho katika michezo, kichupa kidogo kinachozuia nguvu za umeme na sehemu ya katikati ya gurudumu la baiskeli inayoshika gololi. Lugha kopaji ya Kikamba imekopa maana mbili na kuacha maana mbili hivyo kusababisha ufinyizi maana wa leksimu "kikombe".

Neno *suva* katika lugha ya Kikamba hurejelea chombo kilichotengenezwa kwa kioo, sandarusi cha kutilia vitu hasa maji na mafuta. Katika lugha ya Kiswahili, leksimu "chupa" hurejelea kifaa cha kioo cha kutilia vitu hasa maji na mafuta na pia hurejelea sehemu katika tumbo la mwanamke ambayo inafanana na mfuko na ambamo mototo hukulia. Maana ya leksimu "chupa" iliyotoholewa ni moja na hivyo kusababisha ufinyzi maana.

Nomino tulizotalii kwa jumla zinarejelea vifaa ambavyo awali havikupatikana mazingirani mwa lugha ya Kikamba. Ukosefu wa kifaa fulani hufuatilia ukosefu wa leksimu ya kurejelea kifaa hicho. Utohozi maana wa leksimu tulizojadili umeandamana na utohozi wa kifonolojia. Leksimu *landa* ni mfano wa neno lililotoholewa kifonolojia; fonimu [*l*] imechukua nafasi ya fonimu [*r*]. Utohozi huu wa kifonolojia unadhihirisha lugha ya Kikamba kudumisha muundo wa kifonolojia katika maneno mkopo.

#### 3.2.1.2 Mavazi

Vazi ni kitu kama ngozi au nguo kinachovaliwa mwilini. Kwa jumla leksimu zilizokopwa kurejelea mavazi maana msingi ndiyo iliyotoholewa. Leksimu zifuatazo hutumika kurejelea aina tofauti za mavazi.

**(3.5)**

| Kiswahili | | Kikamba |
|---|---|---|
| kaki | > | *kaki* |
| kaputi | > | *kavuti* |
| leso | > | *leso* |
| kilemba | > | *kîlemba* |

Leksimu *kak*i hurejelea nguo ngumu katika lugha ya Kikamba. Katika lugha changizi ya Kiswahili, leksimu "kaki" hurejelea nguo ngumu na pia aina ya mkate. Maana kurejelea vazi ndiyo iliyotoholewa; fahiwa ya leskimu "kaki" imebanika.

*Kavuti* ni neno litumiwalo kurejelea koti zito la kuzuia baridi katika lugha ya Kikamba. Katika lugha ya Kiswahili, leksimu "kaputi" hurejelea koti zito na pia maiti au mfu. Sawa na leksimu *kaki,* maana msingi ya kurejelea vazi ndiyo iliyokopwa. Utohozi huu umesababisha kufinyika kwa fahiwa ya leksimu *kavuti.*

Leksimu *leso* katika lugha ya Kikamba hurejelea vazi la wanawake ambalo hujifunga kiunoni. Katika lugha ya Kiswahili leksimu "leso" hurejelea dhana tatu; kitambaa cha kujifunga kichwani, kitambaa kidogo cha mikononi na vazi la wanawake la kujifunga kiunoni. Maana iliyotoholewa ni maana kurejelea vazi huku maana zingine zikiachwa na kusababisha ufinyizi maana.

Lugha ya Kikamba hutumia neno *Kĩlemba* kurejelea kitambaa au nguo iliyozungushwa kichwani. Katika lugha ya Kiswahili, leksimu "kilemba" hurejelea vitu vitatu tofauti; kitambaa au nguo inayozungushwa kichwani, undu au shungi la jogoo, na pia hurejelea mrungura. Sawa na maneno mengine yaliyotoholewa kurejelea mavazi, maana msingi ya leksimu *Kĩlemba* ndiyo iliyotoholewa.

Mtagusano wa kitamaduni kati ya Wakamba na Waswahili umesababisha kusambaa kwa mavazi miongoni mwa jamii ya Wakamba ambayo awali hayakuwepo. Aidha matukio ya kihistoria kama biashara yalisababisha kusambaa kwa mavazi. Kusambaa kwa mavazi haya kumeandamana na ukopaji wa leksimu ambazo hutumiwa na jamii sambazaji ya Waswahili. Sababu hii imechangia utohozi wa maana msingi kwa lengo la kurejelea vazi



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

lililosambaa huku maana ziada zikipuuzwa. leksimu hizi kwa jumla zinachukua umbo maana la moja kwa moja; yaani dhana inayokusudiwa na wanajamii katika mawasiliano ni moja. Mfano wa neno *leso* unatupa umbo maana la moja kwa moja.

*Leso* ——— vazi livaliwalo na wanawake kwa kujifunga kiunoni.

### 3.2.1.3 Mahali

Neno mahali linatumika katika kazi hii kurejelea sehemu bayana. Ukopaji wa leksimu za mahali umesababishwa na uigaji wa shughulu za kijamii aidha shughuli za kiuchumi au uraibu wa aina fulani. Ukopaji wa shughuli hizi ulisababishwa na mtagusano wa kitamaduni kati ya Wakamba na Waswahili.

| (3.6) | Kiswahili | | Kikamba |
|---|---|---|---|
| | mkahawa | > | *mũkaawa* |
| | baa | > | *mbaa* |
| | kiwanda | > | *kîvanda* |

Neno *mũkaawa* katika lugha ya Kikamba limetoholewa kurejelea mahali panapouzwa chai na vyakula. Katika lugha changizi ya Kiswahili, leksimu "mkahawa" hurejelea hoteli na pia mti uzaao mbuni. Maana ya leksimu "mkahawa" imebanika kwa sababu maana ya mahali ndiyo iliyotoholewa.

*Mbaa* ni neno katika lugha ya Kikamba ambalo hurejelea mahali pauzwapo pombe. Katika lugha ya Kiswahili neno "baa" maana ni pana; kurejelea mahali pauzwapo pombe,

teke la mtu aliye usingizini na kitu kiletacho hasara. Maelezo haya yanaonyesha kubanika kwa fahiwa ya neno “baa”.

Neno *kîvanda* katika lugha ya Kikamba hurejelea banda au mahali pa kufanyia kazi aidha kuuzia bidhaa au kazi nyingine. Katika lugha ya Kiswahili, bali na kurejelea banda la kufanyia kazi, hutumika kurejelea vijiti viwili vya kufungia mtanda katika kazi ya kufuma na pia mayai yaliyipigwa pamoja na chumvi, pilipili, vitunguu. Utohozi maana wa leksimu “kibanda” umesababisha ufinyizi maana wa leksimu hii.

Uchanganuzi wetu unadhihirisha ukopaji uliosababishwa na shughuli za kibiashara zilizoleta jamii mbili pamoja; jamii ya Wakamba na jamii ya Waswahili. Maana zilizotoholewa ni za kimsingi. Utohozi wa kifonolojia pia unadhihirika; kwa mfano neno “mkahawa” fonimu [h] inadondoshwa kwa sababu sauti hii si miongoni mwa konsonanti za lugha ya Kikamba. Kuna utohozi wa kimofolojia pia katika leksimu “mkahawa” ambapo kiambishi *mu* chaongezewa mwanzoni mwa neno.

### 3.2.1.4 Maana Zingine

Maana zingine zimejitokeza katika nomino ambazo hazibainishi waziwazi vitu ambavyo vinarejelewa. Baadhi ni mimea ambayo ilisambaa wakati wa mtagusano kati ya Wakamba na watu wa mwambao wa pwani.

(3.7)

| Kiswahili | | Kikamba |
|---|---|---|
| mzungu | > | *mũũsũngũ* |
| ngano | > | *nganũ* |
| chandarua | > | *kyandalûa* |
| kitanda | > | *kîtanda* |

Neno *Mũũsũngũ* hurejelea mtu wa asili ya Ulaya katika lugha ya Kikamba. Katika lugha ya Kiswahili, neno "mzungu" bali na kurejelea mtu wa asili ya Ulaya, hurejelea tendo la kushangaza na pia mafundisho wapewalo wanawari wakiwa jandoni au unyangoni. Uafafanuzi huu unaonyesha kubanika kwa fahiwa.

*Nganũ* ni leksimu ambayo hurejelea aina ya nafaka katika lugha ya Kikamba. Katika lugha ya Kiswahili, leksimu "ngano" hurejelea aina ya nafaka na pia hadithi. Ukopaji wa leksimu hii umeambatana na kusambaa kwa mmea wa ngano sehemu za ukambani ambao awali haukuwepo. Maana iliyotoholewa ni ile inayorejelea mmea wenyewe. Maana ya pili haikutoholewa kwa sababu katika tamaduni za Wakamba kulikuwepo na kusimuliana hadithi.

*Kyandalûa* ni leksimu ambayo katika lugha ya Kikamba hurejelea aina ya kitambaa kigumu kisichotota maji ambacho hutumika kutengenezea vitu kama mahema. Leksimu *kyandalûa* yatokana na neno la Kiswahili "chandarua". Neno "chandarua" katika lugha

ya Kiswahili hurejelea dhana tatu; kitambaa cha wavu kinachotandikwa juu ya kitanda kuzuia mbu, kitambaa kigumu ambacho hutengeneza mahema na pia hurejelea sehemu ya paa ya motokaa iliyotengenezwa kwa turubali na inaweza kufunguliwa na kufungwa. Ufafanuzi huu unaonyesha kubanika kwa maana ya leksimu "chandarua" kwa sababu maana iliyokopwa ni moja.

Leksimu *kĩtanda* ni mfano wa neno mkopo ambalo wanajamii wa lugha ya Kikamba hutumia kuleta dhana moja. Katika lugha ya Kikamba, leksimu *kĩtanda* hurejelea kifaa cha kulalia na hivyo kurejelea dhana moja. Katika lugha ya Kiswahili, leksimu "kitanda" hurejelea kifaa cha kulalia na pia jeneza na hivyo kurejelea dhana mbili tofauti katika mawasiliano.

Leksimu tulizochanganua bali na kutoholewa kimaana, zimetoholewa kimofolojia. Leksimu *Mũũsũngũ* imetoholewa kimofolojia kwa kuongeza kiambishi *Mũ* ili kuafiki muundo wa ngeli za lugha ya Kikamba

Data iliyokusanywa nyanjani ilidhihirisha mbinu ya ufinyizi maana kuchukua asilimia hamsini ya maneno yaliyokusanywa. Maneno tuliyotalii yamedhihirisha kurejelea vifaa vilivyosambaa eneo la Ukambani kutoka eneo la Pwani. Maoni ya wanaisimu hushikilia kuwa lugha haina budi kukopa maana ambayo awali haikuwepo (Taz Lyons 1877). Jumla ya maneno mkopo mengi ya Kikamba kutoka Kiswahili maana msingi ndiyo iliyotoholewa. Tunaweza kudai kuwa basi mbinu hii imeongozwa na kanuni za kiisimu na kihistoria ambazo uhusika katika unominishaji wa vifaa vipya aidha kupitia

mtagusano wa kitamaduni au mabadiliko ya kiteknolojia. Tulitangulia kusema kuwa lugha hukopa ili kanuni za lugha sizibadilike kupitia ukopaji. Mtazamo huu unaelekeza ukopaji wa maana msingi inayohitajika na wanajamii huku jamii ikiacha maana ambazo hazihitajiki au tayari zimo katika lugha ya Kikamba.

Mtazamo wa Tahakiki Usemi husisitiza kuwa uzalishaji wa matini hudhibitiwa na vikwazo vya kijamii (Taz 1.8.1). Kwa kuzingatia mtazamo huo, vikwazo vya kijamii vimedhibiti kutopanuka kwa maana ya maneno mkopo. Tukumbuke vikwazo vya kijamii uhususha vigezo vya kiisimu pia. Tunatambua maana iliyokopwa na wanajamii wanaitumia kuleta dhana moja katika mawasiliano.

Aidha matumizi ya leksimu kuleta dhana moja katika mawasiliano yanazua maswala ya ualama. Kubanika kwa fahiwa kunamaanisha leksimu mkopo kutumika katika muktadha finyu. Kufinyika kwa muktadha wa leksimu husababisha leksimu hiyo kuwa na ualama msambao. Tunaweza kusema kuwa ufinyizi maana wa leksimu tulizojadili kunabainisha leksimu hizo kuwa na ualama msambao ikilinganishwa na awali, kabla hayajatoholewa kimaana.

### 3.2.2 Usogezi Maana

Usogezi maana uhusisha mfanyiko wa leksimu kupoteza maana awali. Matokeo ya mfanyiko huu husababisha leksimu kuwa na maana tofauti na fahiwa ya awali ya leksimu hiyo (Taz Crowley 1992 na Campbell 1998). Usogezi maana hujitokeza katika namna tofauti:-

1. Sitiari
2. Metonimu
3. Sinedochi
4. Uemeshajimaana
5. Udhalilishajimaana

#### 3.2.2.1 Sitiari

Mbinu ya sitiari hutumika kusogeza maana ya vitu viwili vyenye ufanano. Kitu au kifaa kinachosogezewa maana huwa kina ufanano aidha wa umbo au tabia na kitu awali kilichorejelewa na leksimu husika. Mifano ifuatayo yadhihirisha mbinu ya sitiari.

**(3.8)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| mkoba | > | *mũkomba* |
| maua | > | *Maũa* |
| mtende | > | *Mũũtende* |

Neno *mũkomba* katika lugha ya Kikamba hurejelea kidude kidongo cha kutilia tumbaku. Katika Kiswahili "mkoba" hurejelea mfuko kwa jumla ambao unahusishwa na tamaduni za Waswahili. Ukopaji huu umesababisha kusogea kwa maana ya leksimu "mkoba" na pia athari katika muundo wa kisemantiki. Leksimu *mũkomba* ni kisawe cha neno asili *kĩangi.* Kuwepo kwa leksimu hizi mbili kunaleta maana kuwa zinaweza kutumika katika

muktadha sawa bila matatizo ya mawasiliano. Ukopaji huu umesababisha wanajamii kutumia leksimu mbili kurejelea dhana moja.

**(3.9) Kielelezo cha Kisawe cha Maana.**

*kîangi*

Kifaa kidogo cha kutilia tumbaku

*mũkomba*

Leksimu "maua" ni wingi wa neno ua ambalo ni neno la Kiswahili. Neno "ua" hurejelea sehemu ya mmea inayochanua. Katika lugha ya Kikamba, leksimu *Maũa* imechukua nafasi ya majina ya pekee, kwa kurejelea mwanamke. Katika hali ya kawaida "maua" uhusishwa na urembo. Dhana ya urembo imesogezwa na kuhusishwa na mwanamke.

Neno "mtende" katika lugha ya Kiswahili hurejelea mwanamke au mwanaume mzuri. Katika lugha ya Kikamba neno *Mũũtende* hutumika kama jina la pekee kurejelea mwanamke. Maana ya leksimu "mtende" imesogea kwa sababu katika lugha ya Kiswahili maana yalenga uzuri kwa jumla ilhali katika lugha ya Kikamba maana yalenga jina la mtu hasa mwanamke. Ualama maana pia unatokea kutokana na ukopaji wa leksimu "mtende". Leksimu *Mũũtende* inachukua ualama maana katika lugha ya Kikamba kwa sababu inalenga fahiwa zaidi kuliko leksimu "mtende" katika lugha ya Kiswahili.

Maneno *Maũa* na *Mũũtende* yamechukua nafasi ya majina ya pekee. Aidha mtazamo wa kijamii kuhusisha urembo au uzuri na mwanamke umesababisha usogezi huu. Wanajamii wengi huamini kuwa mwanamke ndicho kiumbe kinachostahili kuwa na uzuri wa tabia au umbo. Kwa jumla nia ya jamii imesababisha usogezi maana wa leksimu *Maũa* na *Mũũtende.*

Uchanganuzi wetu unadhihirisha usogezi maana wa leksimu tulizojadili umesababishwa na ulinganisho wa sifa na umbo. Uzuri wa ua kwa mfano unalinganishwa na uzuri wa mwanamke. Umbo la "mkoba" linalinganishwa na umbo la kifaa asili *Kĩangi* na hivyo maana kusogea.

### 3.2.2.2 Metonimu


Mbinu hii uhusisha mabadiliko ya maana kiasi cha kuhusisha fahiwa zingine ambazo hazikuwa sehemu ya maana awali. Fahiwa ziada kwa kiwango fulani uhusiana na maana awali japokuwa si lazima katika kila hali.

**(3.10)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| kidemu | > | *kĩtemũ* |
| kuandika | > | *kĩandĩki* |
| kambi | > | *Ngambi* |

Neno *kîtemũ* latokana na neno la Kiswahili "kidemu" ambalo hurejelea vazi la kustiri uchi. Katika lugha ya Kikamba, neno *kîtemũ* limesababisha mifanyiko miwili ya kisemantiki. Kwanza, lilitumika kurejelea vazi lililotumiwa kustiri uchi sehemu za nyuma. Vazi asili lililotumika kwa lengo sawa liliitwa *kîtani* ambalo lilitengenezwa kwa kutumia ngozi. Ukopaji wa neno *kîtemũ* ulisababisha usogezi maana wa neno *kîtani* ambalo lilianza kurejelea nguo iliyoraruka na kuzeeka au kitambaa chochote kisichokuwa na umuhimu wa kimavazi. Baadaye neno *kîtemũ* lilibadili maana na kurejelea nguo fupi hasa rinda na pia nguo ambayo imeraruka isiyopendeza machoni. Utohozi wa leksimu *kîtemũ* umesababisha kusogea kwa maana kwa leksimu yenyewe na kukasababisha udondoshaji maana wa leksimu asili *kîtani.*

**(3.11) Kielelezo cha Usogezi na Udondoshi Maana**




Ambapo:

-------------- usogezi maana

__________ maana awali

Maoni ya wahojiwa yalielekeza kuwa, leksimu *kîtani* ndiyo hutumika zaidi kurejelea nguo iliyoraruka na isiyo na maana. Maoni hayo yalituelekeza kutambua kuwa leksimu



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

*kîtemũ* ndiyo yenye ualama msambao kwa sababu hutokea katika muktadha finyu. Maana ya leksimu *kîtemũ* imesogea.

Leksimu *Ngambi* katika lugha ya Kikamba yatokana na neno la Kiswahili "kambi". Neno "kambi" katika lugha ya Kiswahili hurejelea kituo cha safari yaani msafara unapotua na kupumzika na pia hurejelea kituo cha jeshi. Leksimu *Ngambi* katika lugha ya Kikamba hutumika kama jina la pekee kumrejelea mwanaume. Utafiti ulibainisha kuwa jina hili lilizuka kutokana na jina la lakabu ambalo mzee mmoja alijipatia yaani *kambi ya kandû* "kambi ya chakula". Jina hili lilitokana na imani ya mzee huyo kuwa alikuwa mlaji wa chakula kingi na hivyo kuamini yeye alikuwa kambi ya chakula. Utafiti ulibainisha kuwa mzee huyo alikuwa na sifa nyingi kama ulaji wa chakula kingi na pia uzalishaji mali. Kwa sasa jina *Ngambi* ni jina maarufu la ukoo fulani eneo la utafiti.

*Kîandîki* ni neno la Kikamba kutokana na kitenzi cha Kiswahili "andika". Leksimu *kîandîki* hurejelea aina zote za vifaa vya kuandika. Katika lugha ya Kiswahili, kitenzi "andika" hurejelea kufanya alama au michoro kwa kutumia herufi kuwakilisha sauti.

**3.2.2.3 Sinedochi**

Mbinu ya sinedochi husababisha sehemu ya maana ya leksimu kutumika kurejelea maana. Mifano ifuatayo yadhihirisha mfanyiko huu.

(3.12)

| Kiswahili | | Kikamba |
|---|---|---|
| zuia | > | *Asũĩnĩ* |
| kayaya | > | *Kayaya* |
| mto | > | *mũto* |

Leksimu *Asũĩnĩ* latokana na kitenzi "zuia" Neno *Asũĩnĩ* ni jina lakabu lililopewa kundi maalumu kutoka Pwani lililowasaidia Wakamba kuuza pembe za ndovu. Kundi hili ambalo wengi huamini lilikuwa kundi kutokana na Wagiriama lililozuia pembe za Wakamba kutochukuliwa na Waarabu kabla hawajatoa bidhaa za kutosha wakati wa biashara ya *mukuna uku.* Kulingana na historia biashara hii muuzaji na mnunuzi hawakuonana ila waliwasiliana kupitia chuma ambacho baada ya kuacha bidhaa mnunuzi aligonga. Kwa sasa upo msemo usemao *nzou ĩkĩnyĩtwe nĩ mũũsũĩ ndĩthoowekaa* "ndovu ambayo *mũũsũĩ* amekanyaga hainunuliki"; kusisitiza walihakikisha muuzaji aliridhika kabla ya pembe zake kuchukuliwa. Neno hili pia lilipanuka kimaana na kurejelea eneo la pwani *Ũsũĩnĩ*.

Leksimu *kayaya* katika lugha ya Kikamba hutumika kama nomino ya pekee kurejelea mwanamke. Katika lugha changizi ya Kiswahili, neno "kayaya" hurejelea kelele za sherehe. Maana ya kurejelea kelele za sherehe imesogezwa kurejelea mwanamke.

Neno "mto" katika lugha ya Kiswahili hurejelea kitu kama mfuko uliojazwa pamba kinachotumika kuegemezea kichwa wakati wa kulala. Leksimu *mûto* katika lugha ya Kikamba hurejelea kifaa cha kuegemezea mwili mzima wakati wa kulala. Maana ya leksimu "mto" iliyokopwa ni ile ya kuegemezea kichwa wakati wa kulala na kusogezwa kurejelea kifaa cha kuegemezea mwili mzima na wala si sehemu ya mwili. Maana ya *mûto* imesogea kwa kuchukua sehemu moja kurejelea kitu kizima.

#### 3.2.2.4 Etimolojia ya Watu

Mbinu ya etimolojia ya watu, uhusisha mabadiliko ya kimaana kutokana na usawa wa umbo. Neno uhusishwa na neno lingine kimakosa lenye umbo sawa na hivyo kuhusisha usogezi wa maana kimakosa. Mfano unaodhihirisha mbinu hii ni neno *Asomba.*

Neno *Asomba* katika lugha ya Kikamba limenominishwa kutokana na nomino "kusomba" yenye kurejelea kitendo cha kukusanya vitu ovyoovyo. Umbo la neno "kusomba" lakaribiana na neno "Wajomba". Neno "Wajomba" lilitumiwa na Waswahili kuwaita Wamijikenda waliotumiwa na Waarabu katika misafara yao bara. Kimakosa wanajamii wa eneo la utafiti huwarejelea watu wa pwani kama *Asomba* badala ya "Wajomba" Kulingana na wahojiwa, leksimu *Asomba* ilinominishwa nyakati za biashara ya watumwa; yaani kusomba watu ovyoovyo (Taz Ogoti 1976). Utafiti nyanjani ulidokeza kuwa watu kutoka Pwani waliwaambia wenyeji kuwa wamekuja "kusomba" watu Ukambani. Wenyeji walianza kuwaita wageni hao *Asomba* kwa sababu wamekuja kusomba.

### 3.2.2.5 Udhalilikajimaana

Kudhalilika kwa maana ya leksimu ni mbinu ambayo husababisha fahiwa ya leksimu hiyo kuchukua dhana dhaifu katika mawasiliano ya mzungumzaji asili wa lugha. Data ifuatayo ilidhihirisha kudhoofika kwa leksimu mkopo.

**(3.13)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| baraza | > | *valasa* |
| kasuku | > | *kasũkũ* |
| kaniki | > | *kaniki* |

*Valasa* katika muktadha wa lugha ya Kikamba hurejelea kundi la watu, waliokusanyika bila sababu muhimu, wakipiga gumzo lisilo na umuhimu maishani mwao. Wakati mwingine hurejelea mkutano wa kiongozi aidha chifu au mwalimu mkuu. Maana ya kwanza imechukua kudhoofika kwa leksimu hii. Katika lugha changizi ya Kiswahili neno "baraza" hurejelea sehemu, kikundi cha washauri na pia kusanyiko la watu kwa lengo la kuzungumzia mambo yanayowahusu.

"Kasuku" ni neno ambalo katika lugha changizi ya Kiswahili hurejelea aina ya ndege ambaye huiga binadamu. Katika lugha pokezi ya Kikamba, neno *Kasũkũ* hurejelea mtu mwenye maneno mengi yasiyokuwa na msingi.

Leksimu "kaniki" katika lugha ya Kiswahili hurejelea vazi jeusi livaliwalo badala ya kanga wakati wa shughuli za shamba. Neno *kaniki* katika lugha ya Kikamba lilitumika kurejelea vazi jeusi lililovaliwa badala ya kanga wakati wa shughuli za shambani. Maana ya leksimu *kaniki* imedhoofika na kurejelea vazi lililochakaa au vazi lolote jeusi lisilopendeza. Neno *kaniki* hujitokeza katika miktadha ya kufasirika kuwa vazi linalorejelewa halipendezi au ni la zamani na limepitwa na wakati. Tufafanue swala la muktadha kwa kutumia sentensi zifuatazo:

**(3.14) Miktadha Tofauti ya Leksimu *Kaniki***

| | | |
|---|---|---|
| 1. | *Iveti sya kĩlumĩ syĩkĩa tũniki* | kina mama wa *kĩlumĩ* huvalia "kaniki" |
| 2. | *Kowekĩa kaniki?* | Umavalia "kaniki"? |

Sentensi ya kwanza neno *kaniki* linarejelea nguo nyeusi ambazo huvaliwa na kundi la kina mama ambao hucheza ngoma ya kienyeji *kĩlumĩ.* Sentensi ya pili, neno *kaniki* linarejelea nguo ya kawaida nyeusi tititi. Miktadha tuliofafanua yadhihirisha wanajamii wa lugha kopaji ya Wakamba, hufasiri neno *kaniki* kurejelea vazi jeusi lisilopendeza na hivyo kudhoofika kwa mtazamo wa leksimu "kaniki". Tunatambua pia kupanuka kwa muktadha wa lugha katika matumizi ya leksimu *kaniki.*

### 3.2.2.6 Uemeshajimaana

Uemeshajimaana wa leksimu ni kinyume cha udhalilikajimaana. Maana ya leksimu hufasiriwa kuwa na maana bora miongoni mwa wanajamii kuliko awali. Utafiti nyanjani ulibaini leksimu *matumbo* kutokana na "tumbo" imechukua mbinu hii. Neno "tumbo"

katika lugha ya Kiswahili hurejelea sehemu yenye umbo kama mfuko iliyomo ndani ya mwili wa kiumbe na ambayo hufanya kazi ya kupokea chakula na kuanza kukisaga. Neno *matumbo* katika lugha ya Kikamba hurejelea chakula kilichotengenezwa aidha kwa utumbo wa mbuzi au ng'ombe. Chakula *matumbo* huleta dhana bora zaidi kuliko utumbo wa mnyama katika hali ya kawaida.

Ufafanuzi wa leksimu tulizopitia unabainisha kuwa mbinu ya usogezi maana imechangiwa zaidi na vigezo vya kijamii na vigezo vya kiisimu. Mtazamo wa jamii kuhusu neno fulani umesababisha neno hilo kuambatishwa maana fulani huku maana ya zamani ikifutiliwa mbali. Kuwepo na uhusiano dhahania kati ya kiashiria na kiashiriwa kumesababisha jamii ya Wakamba kubadili maana ya leksimu mkopo.

### 3.2.3 Upanukaji

Mbinu ya upanukaji husababisha leksimu kuwa na maana zaidi ambazo hutumika sambamba na maana awali. Utafiti ulibainisha makundi mawili ya nomino zilizodhihirisha upanuzi maana:

1. Maana za kawaida
2. Maana maalumu

#### 3.2.3.1 Maana za Kawaida

Nomino hizi zimechukuliwa kama zile ambazo hazibainishi waziwazi vitu ambavyo vinarejelewa.

**(3.15)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| kahawa | > | *kaawa* |
| sanduku | > | *îsandûkû* |
| chokaa | > | *sokaa* |
| mkeka | > | *mûkeka* |

*Kaawa* ni leksimu ya Kikamba kutokana na neno la Kiswahili "kahawa". Neno *kaawa* hutumika kurejelea vitu viwili: kinywaji na mti wa mkahawa. Katika lugha ya Kiswahili leksimu "kahawa" hurejelea kinywaji kitengenezwacho kwa unga wa buni. Tunatambua kuwa utohozi maana wa leksimu "kahawa" umesababisha upanuzi maana kwa sababu neno *kaawa* larejelea kinywaji na aina ya mti. Leksimu "kahawa" hautumiki kurejelea aina ya mti katika lugha changizi ya Kiswahili. Utohozi maana wa leksimu "kahawa" umepanuka kwa kuhusisha maana kinywaji na maana ya mti.

*Sokaa* ni leksimu ambayo yatokana na neno "chokaa". Leksimu "chokaa" katika lugha ya Kiswahili hurejelea aina ya unga mweupe upakwao kuta za nyumba. Neno *sokaa* katika lugha ya Kikamba hurejelea aina ya unga mweupe upakwao kuta za nyumba na pia

hurejelea chaki au choki: kifaa namna ya kalamu ya udongo kinachotumiwa kuandikia ubaoni. Matumizi ya leksimu *sokaa* katika lugha ya Kikamba huzua fasiri mbili kinyume na fasiri zinazozulika katika lugha ya Kiswahili. Maana ya leksimu "chokaa" imepanuka kwa kurejelea kifaa chaki na unga mweupe. Tunaweza kudai kuwa, leksimu *kaawa* na *sokaa* zimepanuka kimaana na kusababisha kuwemo kwa uhusiano wa polisemia.

**(3.16) Vielelezo vya Polisemia.**

*Kaawa* → kinywaji / Mkahawa

*Sokaa* → Unga mweupe upakwao kuta za nyumba / Chaki; kifaa cha kuandikia ubaoni

Leksimu *îsandûkû* katika lugha ya Kikamba hurejelea kasha la mbao au chuma la kuhifadhia vitu kama nguo, dawa au vitabu na pia hurejelea jeneza. Katika lugha ya Kiswahili, neno "sanduku" hurejelea kasha la mbao au chuma la kuhifadhia vitu. Tunatambua kuwa maana ya neno "sanduku" imepanuka na kuhusisha maana ya jeneza kinyume na awali. Kupanuka kwa leksimu *îsandûkû* kumesababisha leksimu hiyo kutokuwa na ualama msambao ikilinganishwa na awali Yaani, leksimu kutumika katika muktadha mpana zaidi kuliko awali.



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

Neno *mũkeka* katika lugha ya Kikamba hurejelea aina tofauti za mikeka; zulia, mkeka, na *îsenga*. Leksimu "mkeka" katika lugha ya Kiswahili herejelea kitu kama jamvi kinachoshonwa kutokana na kili za miyaa na hukaliwa. Leksimu "zulia" katika lugha ya Kiswahili hurejelea kitu kama mkeka kilichotengenezwa kwa kitani, pamba au sufi ambacho hutandikwa chini. Neno *îsenga* hutumika katika lugha ya Kikamba kurejelea aina ya mkeka asili utengenezwao kwa chane za mti uitwao *mûlala.* Tunatambua kuwa utohozi wa leksimu "mkeka" umefanyika kurejelea aina zote za vitu vya kukalia au kutandikia. Leksimu *mũkeka* inapotamkwa, mzungumzaji asili wa lugha ya Kikamba huwa na fasiri nyingi na tofauti katika mawasiliano kinyume na dhana ambazo hufasiriwa na neno "mkeka" katika lugha ya Kiswahili.

### 3.2.3.2 Maana Maalumu

Nomino hizi hutaja kitu fulani kwa kutumia jina lake moja kwa moja. Kwa njia hii hukitambulisha kitu hiki waziwazi kutokana na kitu kingine chochote cha aina yake.

**(3.17)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| rinda | > | *îlinda* |
| bahati | > | *Vaati* |
| siasa | > | *Siasa* |
| kura | > | *Kũla* |
| karani | > | *Kalanî* |
| mwalimu | > | *Mwalimû* |

*Îlinda* ni leksimu ambayo imetoholewa kutokana na neno "rinda" la Kiswahili. Neno "rinda" katika Kiswahili hurejelea kanzu ya kike iliyo pana. Katika lugha ya Kikamba, neno *îlinda* bali na kurejelea vazi la kike, hutumika pia kurejelea mtu yaani jina la pekee la kumrejelea mtu. Neno *îlinda* linapotumika kumrejelea mtu huwa katika hali ya wingi yaani *Malinda.* Matumizi ya leksimu "rinda" yamepanuka kwa sababu leksimu hiyo inarejelea vazi na pia mtu baada ya kutoholewa.

Leksimu "bahati" katika lugha ya kiswahili hurejelea jambo jema. Katika lugha ya Kikamba neno *vaati* hurejelea jambo jema na pia hutumika kama jina la pekee la kumrejelea mtu hasa wanaume.

*Siasa* ni leksimu ambayo imepitia mfanyiko sawa wa kisemantiki na leksimu *vaati.* Katika lugha changizi ya Kiswahili neno "siasa" hurejelea mfumo wa mawazo wa kuendesha maisha kwa jumla. Katika lugha pokezi ya Kikamba maana msingi imetoholewa. Maana imepanuka kurejelea mtu kama nomino ya pekee; yaani wapo watu ambao huitwa Si*asa.*

"Kura" ni leksimu ambayo hurejelea shughuli za kumchagua kiongozi katika lugha changizi ya kiswahili. Maana ya msingi imetoholewa na pia leksimu *kula* hutumika kama nomino ya pekee yaani jina la mtu. *Kula* ni jina ambalo hurejelea mwanaume miongoni mwa jamii iliyohojiwa.

Neno "karani" katika lugha ya Kiswahili hurejelea mtumishi anayefanya kazi inayohusiana na kuandika ofisini. Katika lugha ya Kikamba neno *kalanĩ* limetoholewa kumaanisha mtu anayefanya kazi ofisini ya kuandika na pia hutumika kama jina la pekee yaani wapo watu waitwao *kalanĩ.* Chanzo cha utohozi wa leksimu *kalanĩ* kama jina kilitokana na kuwarejela waliofanya kazi ya ukarani. Jina *kalanĩ* limepokezanwa kutoka kizazi hadi kizazi na waitwao *kalanĩ* kwa sasa si sharti wawe wanafanya kazi ya ukarani. Jina *kalanĩ* hurejelea wanaume.

Leksimu "mwalimu" katika lugha ya Kiswahili hurejelea mtu afundishaye elimu au maarifa fulani. Utohozi wa neno *mwalimû* umepitia mfanyiko sawa na neno *kalanĩ*; yaani kurejelea mtu afundishaye na pia wapo watu ambao huitwa *Mwalimû* pasipo wao kufanya kazi ya ualimu. Sawa na jina *Kalani*, jina *Mwalimû* hurejelea wanaume.

Uchanganuzi wetu unatuelekeza kutambua kuwa asilimia kubwa ya upanukaji maana watokana na kusambaa kwa kazi tofauti. Historia yatufafanulia watu wa kwanza kupata ajira walikuwa wanaume. Majina mengi kutokana na kazi tofauti yanarejelea wanaume: *Siasa, Kula, Kalanĩ* na *Mwalimû.* Utohozi wa majina umesababishwa na mtagusano wa kitamaduni na hivyo kanuni za kihistoria zimechangia upanukaji maana.

Majina mengine yasiyohusiana na kazi za kiofisi yalizuliwa kutokana na mtazamo wa jamii kuhusu lugha ya Kiswahili. Waliokienzi Kiswahili walijaribu kuyatumia maneno ya Kiswahili kurejelea watu huku sababu msingi ikiwa kustaarabika.

### 3.2.4 Urari wa Umbo

Mbinu ya urari umbo husababisha lugha kopaji kukopa maana peke yake pasipo kukopa umbo la leksimu husika. Maana iliyokopwa huambatanishwa na umbo asili ambalo halikuwa na maana hiyo awali (Taz Anttila 1977). Utafiti ulibainisha kuwa mbinu hii imejitokeza kwa sababu ya ukopaji wa teknolojia ambayo yakaribiana na teknolojia asili. Data ifuatayo ilidhihirisha mbinu hii.

**(3.18)**

| **Kiswahili** | | **Kikamba** |
|---|---|---|
| mbuzi | > | *mbũi* |
| kinu | > | *kĩthii* |

Maana asili ya neno *mbũi* katika lugha ya Kikamba hurejelea mnyama mbuzi. Maana iliyokopwa kutokana na leksimu ya Kiswahili mbuzi ni kifaa cha kukunia nazi. Leksimu *mbũi* hufasiliwa kuwa na maana mbili katika eneo la utafiti na wala si maeneo mengine ya Ukambani (Taz 2.3.2). Dhana moja imesababishwa na maana asili ilhali dhana ya pili imesababishwa na maana mkopo.

*Kĩthii* katika lugha ya Kikamba ni leksimu inayotokana na nomino *ĩthii*. Leksimu *ĩthii* ilitumika kurejelea jiwe kubwa na lingine ndogo. Zamani watu Ukambani walitumia *ĩthii* kusaga unga. Kifaa "kinu" kilipojipenyeza katika utamaduni wa Wakamba, kiliambatishwa jina *kĩthii* kwa sababu kilitekeleza kazi sawa na *ĩthii.*

Uchanganuzi wa urari umbo unabainisha kuwa lugha ya Kikamba imejitahidi kutohoa maneno machache iwezekavyo. Jaribio hili limesababisha matumizi ya leksimu asili kurejelea teknolojia geni.

**Hitimisho**

Sura hii kwa jumla ilijadili na kufafanua kanuni na taratibu mbalimbali za utohozi maana. Uchanganuzi ulibaini kanuni tatu ambazo zinaweza kuhusishwa na utohozi maana wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Kanuni zilizobainika ni: kanuni za kiisimu, kanuni za kijamii na kanuni za kihistoria. Aidha kanuni zilizobainishwa zilionekana kuelekeza mbinu msingi nne za utohozi maana wa maneno ya Kikamba kutoka Kiswahili. Taratibu zilizochanganuliwa ni; ufinyizi maana, usogezi maana, upanuzi maana na urari wa umbo.

Kanuni za kiisimu zilihusisha mfumo wa lugha ambao huwezesha lugha kukua kadri wakati unapopita. Lugha ya Kikamba kama lugha nyingine yoyote ilibidika kuleksisha vifaa vilivyotokana na teknolojia ngeni ambayo ilisababishwa na mtagusano wa kitamaduni. Kuleksisha vifaa au dhana ngeni kulionekana kudumisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Ufafanuzi umebainisha ukopaji wa maana msingi kwa lengo la kukidhi haja ya mawasiliano. Kigezo cha polisemia kimeonekana kusababisha uwezekano wa jamii ya Wakamba kusogeza maana ya baadhi ya maneno mkopo.

Kanuni ya pili ilikuwa ya kijamii. Uchanganuzi ulibainisha kuwa mfumo wa jamii umefungamanishwa na mfumo wa lugha ya jamii husika. Tulitambua kuwa shughuli za jamii ya Wakamba za kila siku kama vile imani, miiko, mavazi na yote jamii inayothamini zimeathiri moja kwa moja maana ya maneno mkopo katika mawasiliano. Aidha maana ya leksimu ilibainika kusogea kutegemea mtazamo wa jamii ya Wakamba. Maneno yaliyopata umaarufu miongoni mwa jamii hii, matumizi yake katika muktadha yalipanuka.

Kanuni za kihistoria zimesababisha mtagusano wa kitamaduni. Ukopaji wa dhani ulidhihirika ambao umesababisha ukopaji wa leksimu za kurejelea dhana hizo. Matukio ya kihistoria ambayo yalidhihirika ni biashara. Dhana za kibiashara zilikopwa kurejelea shughuli hizo za kibiashara. Imani ya Kiislamu pia ilisambaa sambamba na shughuli za biashara. Imani hii imesababisha ukopaji wa dhana za kidini na pia vifaa vya kitamaduni ambavyo viliandamana na dini hii.

Mbinu ya ufinyizi maana ilifafanuliwa. Utafiti ulibainisha kuwa asilimia kubwa ya maneno mkopo yamefuata mbinu hii. Mbinu ya usogezi maana ilibainika kujitokeza katika aina tano: sitiari, metonimu, sinedochi, udhalilikajimaana na uemeshajimaana. Kwa jumla mbinu ya usogezi imesababishwa na kanuni za kijamii na kiisimu. Upanukaji ulionekana kuegemea zaidi nomino za pekee. Leksimu nyingi zilizopanuka zilionekana kutokana na kazi za ujira za kwanza kwanza zilizopatikana miongoni mwa jamii husika. Aidha waajiriwa wa kwanza walikuwa wanaume na ndiyo sababu majina yanayotokana

na kazi mbalimbali yametumiwa kurejelea wanaume. Juhudi za lugha ya Kikamba za kukopa maneno machache zilizosababisha mbinu ya urari wa umbo. Maneno asili yalionekana kukopa maana kutoka lugha ya Kiswahili kwa njia ya kutohoa maana pasipo kutohoa umbo.

Aidha maneno mkopo kutoka Kiswahili yalionekana kujumuishwa katika vikoa maana asili. Baadhi ya maneno mkopo yalichukua nafasi ya ualama maana ikilinganishwa na hali awali; maneno mkopo kutumika kulenga fahiwa zaidi baada ya kutoholewa. Maneno mengine ya mkopo yalionekana kupoteza ualama msambao hasa baada ya kupanuliwa kimaana; neno kutumika katika muktadha mpana baada ya kutoholewa kimaana.

Kazi hii imebainisha kuwa zipo kanuni bia ambazo zimetekeleza taratibu za utohozi maana wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Kanuni hizi hukamilishana katika kufanikisha jaribio la kutohoa maneno kimaana. Jamii ni kigezo muhimu katika ufasiri wa maana. Jamii hukopa ili kukidhi mahitaji ya kiisimu na mahitaji ya jamii yenyewe kama mfumo.

# SURA YA NNE

# HITIMISHO

## Kitangulizi

Utafiti huu ulidhamiria kuchunguza utohozi maana wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Kutotafitiwa kwa kanuni zinazoelekeza taratibu za utohozi maana kiwango cha kuridhisha kulichochea utafiti huu. Pili, taratibu za utohozi maana katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili ziliangaziwa kwa lengo la kufafanua zaidi kanuni zilizotekeleza taratibu hizo. Tatu, athari za kimuundo wa kisemantiki zilizosababishwa na utohozi maana zilijadiliwa. Utafiti ulinuia kuangazia mfumo wa maana ili kuleta ufahamu zaidi katika taaluma ya semantiki na hasa semantiki ya Kikamba.

Uchanganuzi wetu ulijikita katika nadharia changamano; Tahakiki Usemi kama nanga ya utafiti, na Sarufi Amilishi Mfumo kama kijalizo. Tahakiki Usemi hutazama lugha kama usemi. Usemi nao hutazamwa kama mchakato mpana unaovuka mipaka ya kiisimu na kuhusisha vipengele kama tabia, mahusiano, itikadi, mazungumzo, kusoma na kuandika ambavyo vimekubaliwa na kundi maalumu la jamii. Tunaweza kusema kuwa usemi ni mbinu za kujiendesha kimaisha na hivyo ni zao la kijamii; yaani ni mfumo unaoendeshwa na kudhibitiwa na wanajamii.

Usemi kama zao la jamii hujumuisha michakato miwili: uzalishaji matini na utafsiri matini. Utafsiri wa matini huangazia vipengele vitatu muhimu: jinsi muundo wa matini unavyojidhihirisha kiisimu, jinsi matini zinavyojifungamanisha na tatu, uzoevu wa kijamii na mfumo wa kijamii unaohusika na kuzalisha, kusambaza na kutumikiza matini na ambao huelekeza mkondo wa jinsi matini huundwa, kuzungushwa na kutumika.

Mtazamo wa Tahakiki Usemi unatuelekeza kutambua kuwa nanga ya Tahakiki Usemi ni usemi huku uzito ukitiliwa uchanganuzi wa matumizi lugha na jinsi ruwaza za maana huundwa kupitia mchakato wa kijamii. Uchanganuzi wowote basi unaoongozwa na Tahakiki Usemi sharti utilie maanani muktadha wa kijamii katika kutalii maana ya maneno. Kuhakikisha uchanganuzi wa maana umefuata michakato iliyopendekezwa, Tahakiki Usemi imependekeza hatua tatu ambazo zimetumika katika utafiti wetu kama mihimili: maelezo ya milki za matini kulingana na kanuni za kisarufi, ufasiri wa matini kwa kuzingatia kanuni za matumizi lugha kulingana na msikilizaji na tatu ufasili wa matini kulingana na kanuni za muktadha wa kijamii.

Uchanganuzi wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili ulifanyika kwa kuzingatia fasili za wanajamii husika. Msemaji wa lugha ya Kikamba alieleza fasiri tofauti za maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili jinsi yanavyotumika katika ulimwengu halisi wake na wenzake. Fasiri hizi zilizingatia ruwaza za kimaana zinazokubalika na kutumika na wanajamii waliolengwa katika utafiti. Fasiri za maana zilizojadiliwa ni ukubalifu wa wanajamii katika eneo la utafiti; Kitui Kati na Kitui Kusini. Nadharia ya

Tahakiki Usemi iliongoza utambuzi wa maana tofauti za leksimu mkopo kwa kutilia maanani muktadha wa kijamii unaofungamanisha pia vigezo vya kiisimu.

Sarufi Amilishi Mfumo hutazama lugha na matumizi sawa na sheria za kisarufi zinazoshirikiana na ujuzi wa mahusiano ya kijamii. Mtazamo huu huchunguza lugha kama mfumo wa maana, ambao unawakilishwa katika matini za kisarufi na hutambua mawanda matatu: sintaksia, pragmatiki na semantiki, nanga yake ikiwa ni semantiki.

Tanzu hizi tatu za Sarufi Amilishi Mfumo hujikita katika aina tatu za maana: maana tambuzi, maana tagusani na maana matinishi mtawalio. Kipashio cha uchanganuzi katika nadharia hii ni kishazi ambacho kinaweza kutafsiriwa kama sentensi sahili. Mitazamo hii tofauti ya maana pamoja na kishazi ni mihimili thabiti iliyotumika katika utafiti huu. Tulidokeza kuwa maana ya leksimu hujitokeza kwa uangavu, muktadha wa lugha unapozingatiwa. Mtazamo huu ulitumikisha nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo kuongoza utambuzi wa maana ya maneno katika matumizi ya lugha inayokubalika kisarufi. Nadharia ya Sarufi Amilishi Mfumo ilichangia utafiti kwa kuweka leksimu zilizolengwa kuchanganuliwa katika matini mwafaka ambazo zilitumika kuangazia maana ya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Miktadha tofauti ya lugha, ilibaini matumizi mapana ya maneno mkopo yaliyochanganuliwa.

Utafiti huu ulihusisha njia mbili za uchanganuzi: utafiti wa maktabani na utafiti wa nyanjani. Utafiti maktabani ulihusisha udurusu wa vitabu mbalimbali, majarida na tasnifu

mwafaka. Usomi maktabani ulitoa mwangaza kuhusu mada ya utafiti; yaliyoandikwa kuhusu mada na hatua mwafaka za utafiti nyanjani. Utafiti wa maktabani pia ulichangia nadharia bora kuongoza utafiti. Usomi maktabani pia ulibaini hatua za uchambuzi na mbinu za uchanganuzi data. Mtandao maktabani ulichangia usomi kuhusu mbinu na mada zinazohusiana na mada ya utafiti za hivi karibuni.

Nyanjani utafiti ulihusu ukusanyaji wa data kutoka kwa wahojiwa eneo la Kitui Kati na Kitui Kusini. Wahojiwa walikuwa vikundi viwili: wazee kati ya umri wa miaka sabini na juu walio na tajiriba ya lugha ya Kikamba, na kundi la pili lilijumuisha vijana kati ya umri wa miaka thelathini na tano na umri wa miaka arobaini na tano. Jumla ya wahojiwa thelathini na sita walihojiwa. Data iliyokusanywa nyanjani ilitokana na wahojiwa. Data nyingine ilikusanywa kupitia mbinu ya mshiriki mkaguzi hasa sehemu ya mji wa Kitui iitwayo Majengo. Mazungumzo na mahojiano mbalimbali yalirekodiwa kupitia kinasa sauti huku mazungumzo mengine yakinakiliwa na msaidizi wa mtafiti. Simu ya mkono ilitumika hasa kuafiki aslimia ya wahojiwa walioshikilia wazo sawa; yaani wazo kuhusu maana ya leksimu fulani.

Uchanganuzi wa maana ya maneno yaliyokusanywa nyanjani uliongozwa na maswali, majibu na maelezo mbalimbali ya wahojiwa. Uchanganuzi huu pia uliongozwa na matumizi ya maneno hayo yaliyosikilizwa kupitia mbinu ya mshiriki mkaguzi. Tajiriba ya lugha ya Kikamba ya mtafiti pia ilichangia katika uchanganuzi wa maana ya maneno



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

yaliyokusanywa. Taarifa kuhusu mafanikio ya uchanganuzi inadhihirika katika muhtasari ufuatao wa matokeo ya utafiti.

## 4.1 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanahusu uchanganuzi wa kanuni zinazohusika katika taratibu za utohozi maana. Kando na hayo, taratibu za utohozi maana zimefafanuliwa. Matokeo mengine yaliyodhihirika ni sifa za lugha ya Kikamba zinazohusu fonolojia, mofolojia na semantiki. Uchanganuzi wetu ulionyesha kuwa kuna ubunifu mahsusi unaotawala utohozi maana mawanda yote matatu ya kiisimu yaani yale ya fonolojia, mofolojia na semantiki.

Matokeo yalidhihirisha kuwa utohozi wa maneno mkopo ulijitokeza viwango vyote vya lugha; fonolojia, mofolojia na semantiki. Leksimu zilizokopwa na lugha ya Kikamba kutoka lugha ya Kiswahili zilibadili muundo wa kifonolojia na muundo wa kimofolojia. Udondoshaji wa fonimu ambazo hazipatikani katika lugha ya Kikamba ulionekana. Upachikaji na udondoshaji wa viambishi ulidhihirika kutegemea viambishi vya ngeli. Vimbishi pia vilionekana kupachikwa katika leksimu mkopo ili kudumisha muundo wazi wa silabi za lugha ya Kikamba. Uundaji wa nomino kutokana na maneno ya Kiswahili ulionekana kufuata muundo wa kimofolojia wa lugha ya Kikamba. Uchanganuzi kiwango cha semantiki ulibainisha maneno mkopo hutoholewa kimaana, na hivyo kuelekeza uchanganuzi wa data kutoka nyanjani ambayo ilibainisha malengo ya utafiti.

Utafiti huu umeweza kuchanganua kanuni tatu: za kiisimu, kijamii na kihistoria. Kanuni za kiisimu zilidhihirika kuendesha baadhi ya taratibu za utohozi maana. Utafiti ulibaini kuwa, unomishaji ni mojawapo ya kigezo cha kiisimu ambacho huchangia maana za leksimu. Mchakato huu wa lugha umepelekea kuleksishwa kwa bidhaa zilizosambaa kutoka lugha changizi ya Kiswahili hadi lugha pokezi ya Kikamba. Lengo mahsusi la mchakato wa unomminishaji ni kuvipa vifaa vigeni katika lugha nomino za urejeleaji ili kufanikisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii. Jaribio la kurejelea kifaa kigeni, umesababisha maana lengwa kutoholewa huku maana ziada zikipuuziliwa mbali. Jambo hili limesababisha ufinyizi maana.

Hali ya lugha ni kigezo kingine cha kiisimu ambacho kimedhihirisha kusababisha taratibu za utohozi maana. vipengele viwili vya hali ya lugha vilibainika kueleza taratibu za utohozi maana. Uchanganuzi wetu ulidhihirisha hali ya maneno kuwa polisemiki huyawezesha kupanuka au kubanika kimaana. Taratibu za utohozi maana zilizochanganuliwa zilidhihirisha baadhi ya maneno mkopo yalipanuka kimaana na kutumika katika muktadha mpana kuliko awali. Kubanika kwa fahiwa pia kulidhihirishwa ambapo maana ya neno mkopo inafinyika na matumizi ya kimuktadha kuwa finyu. Kwa jumla kipengele hiki kimesababisha ufinyizi na upanukaji maana.

Unasibu wa alama za kiisimu ulionekana kuelekeza taratibu ya usongezi maana. Jamii kopaji ya lugha ya Kikamba haikuwa na sababu za kiisimu za kutotumia neno mkopo kurejelea kitu chochote mazingirani mwake. Kuwepo na uhusiano wa kidhahania kati ya

kirejeleo na kirejelewa katika ulimwengu halisi kulionekana kusababisha usongezi maana wa maneno mkopo.

Kanuni za kijamii zilifafanuliwa na kubainika kuwa vigezo kama nia ya jamii, desturi na dini vimechangia taratibu za utohozi maana. Mtazamo wa jamii kuhusu neno fulani husababisha umaarufu au kudidimia kwa neno hilo katika mawasiliano. Mtazamo wa jamii basi huelekeza kudhalilika kwa neno fulani au kuimarika kwake. Uchanganuzi wa taratibu za utohozi maana ulidhihirisha baadhi ya maneno mkopo kupata umaarufu miongoni mwa jamii kopaji ya lugha ya Kikamba na hivyo kusababisha upanukaji maana. Mtazamo wa kudunisha wa jamii umesababisha kudhalilika kwa maana kwa baadhi ya maneno mkopo katika mawasiliano.

Jamii iliyofanyiwa utafiti ilidhihirisha kuwa na desturi ya kutotaja wakwe na mashemeji kwa jina. Desturi hii yabainika miongoni mwa jamii nyingi. Jambo hili lilionekana kusababisha ukopaji wa "kiholela" mradi jina badala lipatikane kumrejelea mtu wa ukoo ambaye hastahili kutajwa kwa jina lake. Ukopaji huu wa kiholela ulionekana kuchangia usongezi maana.

Dini ni kipengele kingine cha kijamii ambacho kimechangia taratibu za utohozi maana. Utafiti ulidhihirisha kusambaa kwa dini ya Kiislamu eneo la utafiti kumeandamana na kusambaa kwa lugha ya Kiswahili. Kutokana na hali ya kuenzi dini hii, wanaoifuata huenzi lugha ya Kiswahili na kusababisha matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili.

Matumizi mapana ya Kiswahili yamesababisha kupanuka maana kwa baadhi ya leksimu mkopo.

Kanuni za kihistoria zilionekana pia kuchangia taratibu za utohozi maana. Utafiti ulidhihirisha matukio ya kihistoria ambayo yalisababisha mtagusano wa jamii ya Wakamba na Waswahili. Kimsingi, sababu kuu iliyoanzisha mtagusano huu ilikuwa biashara. Jamii pande zote mbili zimekuwa zikibadilishana bidhaa kwa kipindi kirefu. Bidhaa nyingi zilionekana kutoka upande wa Uswahilini hadi Ukambani. Kusambaa kwa bidhaa Ukambani kuliandamana na mchakato wa kuzinominisha bidhaa hizo. Michakato ya kiisimu ambayo tumejadili ilitumika kuleksisha bidhaa geni Ukambani.

Licha ya kusambaa kwa bidhaa kutokana na mtagusano, mtagusano wa kitamaduni pia ulidhihirishwa na utafiti. Tamaduni zinapotagusana, ukopaji wa leksimu sharti utokee katika misingi ya kitamaduni. Mtagusano wa kitamaduni ulisababisha ukopaji wa mavazi, vyakula na matukio mengine ya kijamii. Haya yote yaliandamana na ukopaji wa leksimu kurejelea dhana zilizokopwa huku maana msingi ikitoholewa. Matokeo haya yanakubaliana na maoni ya wanaisimu ambao hutazama lugha kama chombo cha kuendeleza utamaduni.

Uchanganuzi wa kanuni unatuelekeza kutambua kuwa kanuni zote za kiisimu, za kijamii na za kihistoria, zimechangia na kukamilishana katika kuelekeza taratibu za utohozi maana ya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili. Leksimu kama *walaî* kutokana

na tamko “wallah!” ni mfano wa usogezi maana ambao kimsingi umechangiwa na kanuni zote tatu. Utafiti ulionyesha kuwa kanuni zote tatu zimefanikisha taratibu za utohozi maana.

Taratibu za utohozi maana za kimsingi zilizochanganuliwa ni ufinyizi maana, usogezi maana, upanukaji maana na urari wa umbo. Uchambuzi ulionyesha mbinu ya ufinyizi maana imechukua asilimia kubwa zaidi katika data iliyokusanywa. Matokeo haya yanaafikiana na tafiti nyingi za kiisimu ambazo zimebaini hali ya lugha kudumisha muundo asili. Kuna ukubalifu wa wataalamu wa isimu kuwa ni rahisi lugha kudondosha sifa ya kifonolojia au kimofolojia kuliko kutohoa sifa geni. Jambo hili hutokea ili muundo wa lugha kopaji usibadilike kupitia ukopaji. Lugha ya Kikamba ilionekana kukopa zaidi maana msingi na kuacha maana zisizohitajika katika mawasiliano ya kila siku au maana ambazo tayari zimo katika lugha asili ya Kikamba. Ukopaji wa maana msingi umesababishwa na kuwepo kwa dhana geni ambazo zahitaji leksimu za kuzirejelea.

Usogezi maana ulionekana kudhihirika katika njia tofauti: sitiari, metonimu, sinedochi, udhalilikajimaana na uemeshajimaana. Mbinu ya sitiari imesababishwa na ufanano wa kiumbo au sifa. Baadhi ya maneno mkopo ya Kiswahili yenye kurejelea vifaa vyenye umbo sawa na vifaa asili, maana ya maneno hayo kopaji imesogea na kurejelea vifaa asili. Maneno yanayotumika katika lugha ya Kiswahili kuashiria uzuri au urembo

yamesogezwa kuashiria uzuri au urembo wa mwanamke. Aidha maneno hayo yametoholewa kuchukua nafasi ya majina ya pekee kurejelea mwanamke.

Metonimu ni mbinu ambayo ilidhihirika katika matokeo yetu. Mbinu ya metonimu ilionekana kulenga zaidi leksimu zinazorejelea mavazi. Aidha mbinu hii ilionekana kusababishwa na ukuaji wa kitamaduni; mavazi yaliyovaliwa zamani kupitwa na wakati. Mavazi hayo ya kizamani kwa sababu hayatumiki tena, leksimu zilizotumika kuyarejelea zilianza kurejelea vitu tofauti huku kukiwa na uhusiano wa karibu wa virejelewa vipya na virejelewa vya zamani. Mtagusano wa kitamaduni pia ulionekana kuchangia mbinu ya metonimu. Aidha leksimu za mavazi ya kitamaduni ambayo hayakusambaa miongoni mwa jamii ya Wakamba leksimu hizo zilisogezwa na kurejelea mavazi tofauti. Kigezo cha ukuaji wa utamaduni na kigezo cha historia ambacho kilionekana kuchangia zaidi mbinu ya metonimu.

Kusogea kwa dhana kwingine kulitambuliwa kupitia mbinu ya sinedochi. Sehemu ya dhana ya leksimu mkopo ilitoholewa kurejela dhana pana katika lugha ya Kikamba. Leksimu chache zilionekana kudhalilika kimaana baada ya kutoholewa kimaana. Kuimarika kwa leksimu mkopo kulidhihirika katika leksimu moja miongni mwa leksimu zilizokusanywa nyanjani. Sababu za kijamii zilionekana kuchangia kudhalilika na kuimarika kwa maana.

Matokeo mengine yalihusu upanukaji maana. Kupanuka kwa maana kulionekana kulenga majina ya kawaida ambayo yamepanuka maana na kuwa majina ya pekee. Aidha vipengele vya desturi ya jamii ya Wakamba na imani ya Kiislamu vilionekana kuchangia zaidi mbinu ya upanukaji maana. Vipengele hivi viwili viliainishwa kama vipengele vya kanuni za kijamii.

Urari wa umbo ni mbinu nyingine katika matokeo ya utafiti wetu. Baadhi ya maneno asili yalionekana kuchukua maana geni kutokana na maneno ya Kiswahili. Maana mkopo zilizoambatanishwa na maumbo asili zilionekana kulenga dhana za kiteknolojia. Mtagusano wa lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili ulisababisha kusambaa kwa vifaa vya kiteknolojia. Vifaa vile vilionekana kuchukua nafasi ya vifaa asili. Aidha leksimu asili ilitumika kurejelea kifaa kipya na pia maana mkopo.

Athari katika muundo wa kisemantiki wa lugha ya Kikamba ni matokeo mengine ya utafiti wetu. Leksimu mkopo zilionekana kusababisha upanukaji wa vikoa maana au udondoshaji wa leksimu asili kutoka kwa kikoa maalumu. Leksimu mkopo pia zilionekana kuathiri dhana ya ualama. Aidha leksimu asili zilionekana kuchukua mkondo wa ualama msambao au ualama maana kutokana na utohozi maana wa leksimu za Kiswahili.

Taratibu za utohozi maana na kanuni zake zimeonekana kuwa mchakato unaozunguka jamii nzima kwa jumla. Aidha mfumo wa lugha ya Kikamba ulionekana kufungama kwa karibu na mfumo wa kijamii. Jamii ya Wakamba imekopa ili kudumisha mawasiliano na kudumisha mahusiano ya kijamii. Ukopaji wa leksimu za lugha ya Kikamba kutoka lugha ya Kiswahili ulionekana kujikita katika msingi mpana wa kijamii; yaani manufaa katika viwango viwili: kiisimu na kijamii.

## 4.2 Mahitimisho ya Utafiti.

Leksimu za Kikamba zilizokopwa kutoka Kiswahili zimetoholewa kimaana. Utohozi maana umetokea ili kuelezea dhana mkopo kutoka lugha ya Kiswahili ambazo hazingeweza kuelezeka wazi kwa lugha ya Kikamba. Zaidi, utohozi maana umesababishwa na vikwazo vya kijamii. Baadhi ya maneno yametoholewa kimaana ili kukidhi mahitaji ya kijamii kama vile miiko. Ukopaji wa maneno na jamii ya Wakamba umedhihirisha ukuaji wa lugha na utamaduni. Historia ndefu kati ya jamii ya Wakamba na jamii ya Waswahili ni kuchochea cha utohozi maana. Falsafa ya jamii ya Wakamba kuhusu lugha ya Kiswahili ilionekana kuchangia utohozi maana hasa upanukaji maana. kwa jumla taratibu za utohozi maana zilizobainishwa ni: upanuzi, ufinyizi, usogezi, na urari wa umbo.

Kanuni tatu zilionekana kuhusika katika taratibu za utohozi maana; kanuni za kiisimu, kijamii na kihistoria. Uchanganuzi ulidhihirisha kuwa kanuni hizi zimeshirikiana pamoja katika kuelekeza maana ya maneno mkopo. Uchambuzi ulionyesha kuwa wanajamii ndio



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

kigezo cha kimsingi katika kufasiri dhana zinazoashiria ulimwengu halisi. Wanajamii hutumia alama za kiisimu kurejelea ulimwengu halisi. Alama za kiisimu tofauti huashiria dhana tofauti kutegemea mtazamo wa jamii husika. Aidha jamii ya Wakamba imetumia maneno mkopo kufinyanga ulimwengu wao kutegemea mtazamo wa jamii hii. Matokeo ya jaribio hili yalionekana kuwa taratibu tofauti za utohozi maana.

Utohozi viwango vyote vya lugha unadhihirisha ubunifu maalumu unaoongoza ukopaji wa maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili.

## 4.3 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Utafiti huu ulichanganua utohozi maana katika maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili kwa kuegemea kanuni za taratibu za utohozi maana. Baadhi ya maneno mkopo yalionekana kubadili maana baada ya kipindi fulani. Swala hili halikushughulikiwa kwa undani kwa sababu za upeo na mipaka ya utafiti huu. Kazi hii inapendekeza utafiti zaidi ili kubainisha mabadiliko ya kisemantiki au etimolojia ya maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili, swala ambalo halijaangaziwa katika mfumo wa lugha ya Kikamba.

Utafiti maktabani ulidhihirisha japo lugha ya Kikamba imetafitiwa kwa kina viwango vya fonolojia, mofolojia na sintaksia, kiwango cha semantiki kimepuuzwa na kusahaulika. Aidha utafiti zaidi kiwango cha semantiki utawapa watafiti wengine katika eneo hili msingi mwafaka kipindi kajacho.

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha mtagusano kati ya lugha ya Kikamba na lugha ya Kiswahili. Ilibainika kuwa, lugha ya Kiswahili pia imekopa maneno kutoka lugha ya Kikamba. Swala hili halikutiliwa maanani kwani lilikuwa kando na upeo wa utafiti wetu. Utafiti zaidi wapendekezwa kwa lengo la kubaini iwapo yapo maneno katika lugha ya Kiswahili yaliyokopwa kutokana na lugha ya Kikamba na jinsi yalivyotoholewa viwango vyote vya lugha. Huenda utafiti huo ukafaa wanahistoria wa lugha ya Kiswahili katika kujumuisha lugha zilizochangia maneno lugha ya Kiswahili.

## MAREJELEO


Anttila, R. 1972. *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics.* Nairobi: Macmillan.

Bynon, T. 1977. *Historical Linguistics*. Cambridge; Cambridge University Press.

Campbell, L. 1998 *Historical Linguistics: An Introduction.* Edinburgh: Edinburgh University Press.

Crowley, T. 1997. *An Introduction to Historical Linguistics 3 Edition*. New York: Oxford University Press.

Cruse, D.A. 2000. *Meaning in Language. An Introduction to Semantics and Pragmatics.* New York: Oxford University Press.

Fairclough, N. 1989. *Language and Power*. New York: Longman Inc.

Fasold, R. 1984. *The Sociallinguistics of Society.* Cambridge: Basili Blackwell Limited.

Habwe, J na Peter Karanja. 2004. *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Halliday, M. A. K. 1985. *An Introduction to Functional Grammar London:* Edward Arnold.

Halliday, M. A. K. 2004. *An Introduction to Functional Grammar 3rd Edition.* London OUP.

Hock, H.H. 1986. *Principles in Historical Liguistics.* Berlin: Mouton de Gruyter.

Hofmann, J.1931 (Makala yaliyopatikana Ikutha African Inland Church. Hayajachapishwa).

htt://www.uonbi.ac.ke

http://citeseer.ist.psu.edu

http://web.as.uky.edu

http://www.linguist.org

Kibrik, A. E.977. *The Methodology of Field Investigations in Linguistics. Netherlands:* Mouton and Co. B. V Publishers.

Kioko, A.N. 2005 *Theoretical Issues in the Grammar of Kikamba A Bantu Language.* Monash: LiNCOM GmbH Publishers.

Kitavi, H.1992. *"*A Comparative Study of the Kitui North and Machakos Dialets of Kikamba*"* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Lehman, W. P. 1962. *Historica Linguistics.* New York: Holt, Rinehart and Winston Inc.

Locke, T. 2004 *Critical Discourse Analysisi.* Amazon Continum International Publishing group.

Lyons, J.1977 *Semantics Volume 1.* New York: Cambridge University Press.

Lyons, J. 1977 *Semantics Volume 2.* New York: Cambridge University Press.

Lyons, J.1981 *Language and Linguistics.* Cambridge University Press.

Massamba, D.2004 Kamusi ya Isimu na Faisafa ya Lugha.Dar-es-Salaam: TUKI

Maundu. 1980 "Sound Change and Reconstruction of Kikamba Consonantal Sounds". Nairobi: Thesis.

Mbaabu, I. 1996. *Language Policy in E. Africa. Nairobi:* ERAP.

Mbaabu, I.*2003* *Sheng - English Dictionary.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Martnet, A.1964. *Elements of General Linguistics*. London: Faber and Faber Ltd.

Mc Mahon. 1996 *Understanding Language Change.* New York: Cambridge University Press.

Mgullu, S. R. 2004. *Mtalaa wa Isimu.* Nairobi: Longhorn.

Mugambi. 2007. "Utohozi Maana Katika Maneno ya Sheng'" Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwihaki, A. N 1998. "Loanword Nativisation: A Genera View of the Gikuyu Loanwords". Tasnifu ya uzamifu Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mwihaki, A.N. 2006 "Sheng" na Usomi wa Kiswahili, Mtazamo wa Kiisimu Jamii". (Makala ya semina ya jamii ambayo yalitolewa Mjini Nakuru. Hayajachapishwa)

Ngesu, S. 2005. "Usimilisho wa Maneno Mkopo ya Kikamba kutoka Kitharaka na Kiswahili". Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ogoti B.A.1976 *Kenya Before 1900*. Nairobi: east African Publishing House Ltd.

Odden, D. 2005. *Introducing Phonology*. New York: University of Cambridge.

Palmer, F. R. 1996. *Semantics 2nd Edition*. Cambridge University Press.

TUKI. 1981 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar-es-Salaam:TUKI

TUKI. 1990. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Dar-es-Salaam:TUKI

TUKI. 1996 *English-Swahili Dictionary*. Dar-es-Salaam:TUKI

Romaine, S. 1994. Language and Society. *An Introduction to Sociolinguistics.* New York: Oxford University Press.

Whiteley, H. 1963. *Loan-Words in Kamba: A Preliminary Survey.* London: University of London.

Whiteley, H. &. Muli, M.C. 1962 *Practical Introduction to Kamba.* Nairobi: Oxford University Press.

## KIAMBATISHO

Yafuatayo ni maneno mkopo ya Kikamba kutoka Kiswahili, yakiwa yameainishwa kutegemea vikoa maana.

**Majina ya watu**

| **Kiswahili** | **Kikamba** |
|---|---|
| rinda | Malinda |
| bahati | Vaati |
| siasa | Siasa |
| kura | Kũla |
| karani | Kalanî |
| mwalimu | Mwalimû |
| kambi | Ngambi |
| Ishmael | Sumaili |
| kayaya | Kayaya |

**Mavazi**

| | |
|---|---|
| wallah! | Walaî |
| kidemu | kîtemû |
| kaniki | kaniki |
| kaki | kaki |
| kaputi | kavuti |
| leso | leso |
| kilemba | kîlemba |

**Mimea**

| | |
|---|---|
| mnazi | mũnathi |
| mtende | mũtende |
| mwembe | mũembe |
| ngano | nganû |

**chakula**

| | |
|---|---|
| mchele | mũsele |
| sukari | sukalî |
| guru | ngũlu |

**wanyama**

| | |
|---|---|
| farasi | mbalasi |
| paka | mbaka |
| nyumbu | nyûmbû |

**Mahali**

| | |
|---|---|
| mkahawa | mũkaawa |
| baa | mbaa |
| kiwanda | kîvanda |

**Nomino zingine**

| | |
|---|---|
| mzungu | mũũsũngũ |
| chandarua | kyandalû |
| kitanda | kîtanda |
| nyanya | înyanya |

| | |
|---|---|
| kimba | kimba |
| maiti | maiti |
| buku | îvuku |
| mkoba | mûkomba |
| kuandika | kîandîki |
| mto | mûto |
| zuia | Asûînî |
| Wajomba | Asomba |
| baraza | valasa |
| kasuku | kasûkû |
| matumbo | matumbo |
| sanduku | îsandûkû |
| chokaa | sokaa |
| mkeka | mûkeka |
| kekee | kekee |
| randa | landa |
| kikombe | kîkombe |
| chupa | suva |



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY